# *KUMWAMINI MUNGU*

Wakati utakuja lini
Nitakapoweka silaha zangu karibu,
Na kukaa kwa amani Nyumbani?

Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Na kisha tunakusanyika Nyumbani!

Hakuna furaha ya utulivu duniani nijuayo,
Hakuna kuba ya amani, makazi;
Ulimwengu huu ni jangwa la ole,
Ulimwengu huu si Nyumbani kwangu.

Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Nasi tutakusanyika Nyumbani.

Kwa Yesu Kristo nilikimbilia nipate raha;
Aliniagiza niache kuzurura;
Na kuegemea kifuani Mwake kwa ajili ya msaada
Mpaka anipeleke Nyumbani?

Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Na tutakusanyika Nyumbani!

Nilitafuta mara moja upande wa Mwokozi wangu,
Hatua zangu hazitatanga-tanga tena;
Pamoja Naye nitastahimili wimbi la baridi la kifo
Na kufika Makazi yangu ya Mbinguni.

Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Tutafanya kazi mpaka Yesu aje,
Nasi tutakusanyika Nyumbani.

2 Nambari 227 sasa, *Kukusanya Miganda Mizuri*. Ninapenda kuimba huu, ni kwa sababu ni wimbo wa kimishenari, na kwa namna fulani—kwa namna fulani hunipa moyo. 227 ndiyo nambari ya wimbo. Vema, sasa, wimbo wa kufunga kab-. . . Sasa hebu, kila mtu, tujiunge nao moja kwa moja sasa. Je, mnapenda nyimbo hizi za kale? Semeni, "Amina," kama mnazipenda. [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ajabu! Vema, sote pamoja sasa:

Leo kwenye mashamba ya mavuno tutaenda kwa furaha,
Kukusanya miganda, loo, miganda mizuri;
Tangu mapema alfajiri mpaka usiku tutafanya kazi kwa nguvu zetu,
Kukusanya miganda, loo, miganda mizuri.

Kukusanya miganda, miganda nzuri,
Kukusanya miganda, miganda mizuri;
Ee, Bwana asifiwe, tuko njiani kuelekea Nchi ya siku isiyo na mwisho,
Kukusanya miganda, loo, miganda mizuri.

Juu ya mlima, vilima au tambarare tutavuna nafaka,
Kukusanya miganda, miganda mizuri;
Ndiyo, tutafanya kazi mbali na karibu, tusilegee, tusiogope,
Kukusanya miganda, loo, miganda mizuri.

3 Kila mtu sasa, twende!

Kukusanya miganda, loo, miganda mizuri,
Kukusanya miganda, miganda ya dhahabu, miganda mizuri ya dhahabu;
Bwana asifiwe, tuko njiani kuelekea Nchi ya siku isiyo na mwisho,
Kukusanya miganda, miganda mizuri.

4 Ngoja kidogo. Sasa tunapokuja kwenye sehemu hiyo tena, “Bwana asifiwe, tuko njiani kuelekea Nchini,” tuelekeze juu, “kwa Nchi ya siku isiyo na mwisho, kukusanya miganda.” Hebu tujaribu pambio sasa. Haya!

Bwana asifiwe, tuko njiani kuelekea Nchi ya siku isiyo na mwisho,
Kukusanya miganda, miganda mizuri.

5 Vema, sasa tuupate tena. Vema.

Tutaimba na tutaomba, na kutii Sauti ya Bwana wetu,
Kukusanya miganda, loo, miganda mizuri;
Tunapokwenda katika nchi za kigeni, tukifanya yale aliyotuamuru Bwana wetu,
Kukusanya miganda, miganda mizuri.

Kukusanya miganda, miganda mizuri,
Kukusanya miganda, miganda mizuri;
Ee, Bwana asifiwe, tuko njiani kuelekea Nchi ya siku isiyo na mwisho,
Kukusanya miganda, miganda mizuri.

Hebu tusimame sasa, tafadhali.

6 Ee Bwana wa Uzima, tunakuona Wewe katika Kitabu kiitwacho Biblia, katika picha ya ajabu, asubuhi ya leo,

kama vile tungefikiria kuwa ni Jumapili nzuri asubuhi ulipokuwa umeketi juu ya mlima, ukawakusanya wanafunzi Wako kukuzunguka na ulikuwa ukiwafundisha katika heri, mambo tu ambayo wanapaswa kufanya. Ulisema, "Heri wenye upole, maana hao watairithi nchi. Heri walio maskini wa roho, maana Ufalme wa Mungu ni wao. Heri ninyi, watu watakapowashutumu, na kuwatesa, na kusema kila aina ya uovu dhidi yenu kwa uongo, kwa ajili ya Jina Langu. Furahini, na kushangilia, kwa maana thawabu yenu ni kubwa Mbinguni."

7 Kwa namna hii, ulitufundisha sote kwamba tunapaswa kuomba hivi:

> Baba yetu uliye Mbinguni, Jina Lako Litukuzwe.
> Ufalme Wako uje. Mapenzi Yako yafanyike duniani, kama yalivyo Mbinguni.
> Utupe leo riziki yetu.
> Utusamehe makosa yetu, kama sisi nasi tunavyowasamehe wanaotukosea.
> Na usitutie majaribuni, bali utuokoe na yule mwovu; Kwa kuwa Ufalme ni Wako, na nguvu, na utukufu, milele. Amina.

8 Sasa madarasa yanaweza kuchukua nafasi zao. Darasa la watu wazima songeni mbele mkiweza, huku wavulana wakitupa *Wingu Na Moto*. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

9 Sasa kuna viti vitupu mbele, ikiwa baadhi yenu mlio nyuma kabisa. Najua maskani yetu siyo. . .sauti hapa si nzuri sana, kwa sababu tuna kuduta kwa sauti kati ya kila moja ya hizo nguzo chomozi hapo, na boriti zinazoning'inia chini. Kuna kurudishwa sauti. Ikiwa unataka kuja karibu, kuna viti vichache. Unakaribishwa hata na zaidi, tunapofanya hivi, ikiwa unataka.

10 Hebu na tufungue sasa kwenye Mwanzo mlango wa 22, na kisha tufungue pia Warumi mlango wa 4, kwa ajili ya u—ujumbe mfupi tu asubuhi ya leo kabla ya ibada ya uponyaji, katika mafundisho yetu ya shule ya Jumapili. Mwanzo 22.

11 Je, kuna mtu anayehitaji Biblia? Ulisahau yako? Kama ulisahau, inua tu mkono wako kama unataka moja ya kusomea. Tunazo kadhaa nyuma hapa. Tutafurahi kuwa na mmoja wa wahudumu kuwaletea moja kwa moja, ikiwa unataka moja. Niliona mikono imeinuliwa. Ndugu Roy, je, nyinyi ndugu tafadhali ingieni kwa dakika moja, mpitishe hizo huko nyuma kupitia hapo. Hiyo itakuwa sawa.

12 Bibi Harvey hapa, Bibi G. H. Harvey kutoka Danville, Illinois? Je, unaye mvulana wako pamoja nawe? Vema. Tutakuwa na maombi baada ya muda mfupi tu, kwa ajili yake. Sawa, Bibi Harvey. Sawa.

13 Sasa tutazungumza kidogo tu, ama kuwa na shule ya Jumapili. Ni kawaida hapa kwamba tuna somo letu la shule ya Jumapili. Lakini nikiwa nyumbani, mbona, kwa kawaida mimi. . .wanakubali na kuniruhusu niwe na shule ya Jumapili, kwa sababu ya kuwaombea wagonjwa. Na ndipo mchungaji wetu ataleta ujumbe wa asubuhi, mara tu baada ya sehemu hii ya ibada. Nasi tutajaribu kumpa jukwaa haraka iwezekanavyo, kufikia saa tano, Bwana mwema akipenda.

14 Sasa kuna haja nyingi. Nami ni—ninawaombea ninyi nyote kila mara, na kila mahali, nami ninawataka ninyi mniombee.

15 Nina kitu, sababu ya kuwa nyumbani kwa muda mrefu wakati huu, ninatafuta njia ya Kiungu ya Mungu ili niende katika ibada zangu zinazofuata, kama nilivyomwahidi ningefanya. Sasa, sijaribu kumharakisha Bwana, maana Yeye anajua mambo yote, lakini ninamwomba anionyeshe ono la kile ninachopaswa kufanya, ama mahali ambapo hatua yangu inayofuata itakuwa. Na tangu nitoke Afrika, kumekuwa na ono moja tu lililotukia, nalo lilikuwa ni asubuhi ile nyingine, kisha ikaja mara mbili au tatu kwa siku. Nami naamini ya kwamba Yuko karibu sasa.

16 Maono kawaida huja kwa lundo. Kama umeona katika Biblia, juu ya. . .ndugu zetu wa siku zilizopita, kwamba kwa kawaida kundi la maono ambayo yangeingia kwa Danieli, au kwa Yusufu, na kisha kungekuwa na ki—kipindi ambacho hakingekuwa na lolote.

17 Mara nyingi nimekuwa nikijiuliza ikiwa ninapaswa kuziendesha huduma zangu jinsi nimekuwa nikiziendesha. Omba tu, loo, labda nipate dazeni, mbili, usiku mmoja, ama kitu kama hicho, ambapo kuna maelfu yao wanangojea, na inaendelea tu kuja moyoni mwangu kwamba sipaswi kufanya hivyo; kwamba, Mungu alikuwa amenipa mamlaka ku—kuweka magonjwa. . .kuvunja nguvu za Shetani.

18 Na Jumatano usiku, juma moja, nilishuka hapa maskanini, na kulikuwa na kundi la watu waliokuwa wamekusanyika, kwa hiyo niliweka tu, kama, manyoya ya kondoo mbele za Bwana. Nami nikasema, “Bwana, sikuwahi kutoka nje. . .”

19 Nimekuwa, mara nyingi, daima nimewauliza watu; kwanza, “Unaamini? Unaamini kiasi gani? Unaamini ninaweza kufanya hivi?” na mambo haya yote tofauti namna hiyo. Na kisha—na kisha ningengoja na kuwaleta jukwaani, na kungoja mpaka nione ono, nione hasa kile kilichokuwa kikiendelea, ndipo ningetamka jinsi ilivyokuwa. Ilikuwa polepole sana, sikuweza kuwafikia watu. Lakini siku chache zilizopita, nilikuwa nikishangaa. . .

20 Mara nyingi, ningekuwa nimesimama jukwaani, ambapo kunaweza kuwa na watu laki moja. Na, jambo la kwanza unajua, kitu fulani cha ujasiri kinainuka ndani yangu, nami

ningeendelea moja kwa moja na kumwita huyo pepo, na kumtoa. Na nilifikiria, "Hiyo ni ajabu." Na halafu hapa ninaanza kufikiria... Wengi wenu mmesoma kitabu changu kidogo, bila shaka nyote humu ndani, na matukio mengi mle.

21 Niliwaona usiku mmoja, kule Portland, ambako pepo... Na, loo, jamani! Mtu mwenye uzito wa pauni mia tatu, karibu hivyo, na kukimbilia jukwaani, naye akasema, "Naam, mnafiki wewe!" Kasema, "Nitakuonyesha ni mtu wa Mungu kiasi gani!" Alikuwa ni mwendawazimu kutoka kwenye taasisi hiyo. Naye akakimbia hadi jukwaani na—na alikuwa anaenda kuvunja shingo yangu. Na—na wahubiri mia tano walikuwa ndio kwanza waanguke kutoka kwake. Naye akavuta mkono wake nyuma akasema, "Nitavunja kila mfupa katika mwili wako!" Nami nilikuwa na uzito wa pauni mia moja ishirini na nane. Naye kama mia tatu, na kifua kikuu kirefu, na, loo, jinsi alivyokuwa m—mtu mwenye nguvu, aliyeweza kabisa kutekeleza vitisho vyake. Na katika... Papo hapo katikati yake, mbona, kulikuwa na kitu fulani tu kilichosogea juu yangu, na nilitoka tu hadi pale alipokuwa. Alisema, "Usiku wa leo nitavunja kila mfupa katika mwili wako unaoonekana dhaifu!"

22 Nikasema, "Ndani ya... Kwa sababu umempinga Roho wa Mungu, usiku wa leo utaanguka juu ya miguu yangu, katika Jina la Bwana."

Kulikuwa na unabii mbili zilizofanywa.

23 Naye akanijia mbio, akasema, "Nitakuonyesha ni miguu ya nani nitakayoangukia!" Naye akanitemea mate usoni alipokuja, naye akavuta nyuma ngumi yake kubwa.

24 Hapo hapo nikasema, "Shetani, toka ndani ya mtu huyu." Naye akainua mikono yake na kupiga mayowe, na akaanguka miguuni mwangu, hata ikabidi polisi wamtoe.

25 Sasa, hakuwa na imani yoyote kwangu. Hakuniamini. Na ninaona inahitaji changamoto ya ujasiri. Nimekuwa nikiombea kila anayekuja.

26 Usiku ule mwingine kulikuwa na watu hapa, mwanamke mmoja asingeweza kuongea. Mara tu nguvu hiyo mbaya ilipopingwa, alizungumza kawaida.

27 Na kulikuwa na mama hapa aliyekuwa na tezi kubwa kwenye koo lake. Nilimwendea tu, na kusema, "Shetani, ni—nina mamlaka tu ya kuvunja nguvu zako. Lazima utoke kwake."

Nikasema, "Ameondoka." Nikasema, "Je, unaamini hivyo?" Naye akasema, "Ndiyo."

28 Nikasema, "Vema, nenda nyumbani na kuweka kamba shingoni mwako, na kuipima, uone ni kubwa kiasi—kiasi gani. Na kila baada ya siku tatu, kata kipande cha uzi kutoka hapo, uone jinsi inavyoanza kupungua."

29 Siku ya kwanza ilikuwa kama kiasi *hicho*, siku ya pili karibu *hivyo,* na siku ya tatu yapata *hivyo,* mahali iliposhuka, unaona. Ni kamba ile ile; aliileta hapa jukwaani.

30 Ndipo nikaanza kuisikia ikiingia. Nami ninamwomba Mungu tu, je, hayo yanaweza kuwa ni mapenzi Yake ya Kiungu? Ndipo hivi majuzi asubuhi yapata . . .

31 Nina msichana mdogo, nane, kumi—umri wa miezi kumi, mtoto Sarah, naye ni maskini kipenzi. Na sijapata kuwa naye sana. Na nimemharibu, nitakubali hilo, ninamshikilia tu mikononi mwangu kila wakati. Ungeweza, pia, ikiwa hungepata kuona penzi hilo dogo zaidi ya vile ninavyopata kumwona, unajua, mara kwa mara ninapokuwa nyumbani. Kwa hiyo na—nadhani nilimharibu sana.

32 Anaota baadhi ya meno, na anaumwa sana. Lazima atakuwa ana ugonjwa wa kuhara damu pia. Unazunguka. Nadhani baadhi ya familia zenu zinao, pia; mgonjwa sana, kutapika na kuhara damu. Na hivyo alikuwa akilia. Mama yake alikuwa amechoka sana, hata hakuamka; wala na mimi, sikuamka. Nami niliamka, na nilikuwa nimelala nyuma katika chumba cha pili kutoka kwake; na mama yake na yeye mle ndani, na mimi na msichana huyo mdogo tulikuwa tumelala katika chumba kingine, mtoto Rebekah. Na, kwa hiyo, na Billy Paul alikuwa anakaa na nyanya yake usiku huo. Kwa hiyo, ni—nikaamka, nikasikia . . . Nilisema, "Ni nini kilinifanya niamke hivyo?"

33 Nilisikia Sauti Yake ikisema, "Nenda kwa mtoto wako na umpe maji ya kunywa."

34 Niliingia chumbani, naye alikuwa analia. Alikuwa amelia kwa muda mrefu. Lazima hakumuamsha mama yake, kwenye maskini kitanda chake cha kulala. Nilienda kuchukua glasi ya maji huku nikiingia ndani. Maskini mtoto huyo karibu alikunywa glasi nzima ya maji, na pale katika hali yake wakati huo, akiwa na ugonjwa wa kuhara damu aliokuwa nao. Nilidhani tu, "Je, hilo si ni la kupendeza, jinsi Yeye ni mwema kufanya hivyo!" Hiyo ni mara ya pili, au mara ya tatu.

35 Wakati mmoja nilipokuwa Sioux Falls, alikuwa na umri wa miezi mitatu tu. Alikuwa amejilaza kitandani. Mama yake alikuwa ametoka nje, akiongea na watu wengine. Nami nilikuwa nikinyoa, namna hiyo, nikijitayarisha kwenda kwenye mkutano. Nami nilikuwa nimesimama pale, nikinyoa, ndipo nikamsikia Malaika wa Bwana akisema, "Mchukue mtoto wako, haraka sana." Niliweka wembe wangu chini; nikakimbia kuzunguka. Na kwa nusu dakika zaidi na angekuwa ameenda. Alikuwa juu ya kitanda kirefu, karibu *hivyo*. Naye alikuwa na mikono yote miwili . . . Alikuwa anajiviringisha tu, na alikuwa amevingirisha kichwa chake, maskini kichwa chake kimening'inia chini, mkono wake, ukiteleza tu. Ilinibidi kukimbia upesi sana kumshika alipoondoka tu. Yeye ni mzuri, wa kupendeza.

36 Baadaye kidogo kutoka hapo, kulikuwa na msichana mdogo. Labda ameketi hapa asubuhi ya leo. Simwoni, lakini yeye huja mara moja moja. Yeye ni mshiriki wa kanisa huko New Albany, kanisa maarufu sana, kanisa maarufu huko New Albany. Nimekuwa huko chini. Yeye anataka. . . Ana ugonjwa wa akili, aina fulani ya kuchanganyikiwa akili. Na yeye hawezi, hata hataondoka jijini au popote, anaanza kupiga mayowe na kulia, akiendelea. Kwa hiyo mimi—mimi nilimwombea, mara mbili au tatu, lakini kitu fulani hakingeniruhusu nimpinge pepo huyo, kwa namna fulani. Sijui. Sikuweza tu kuifanya. Yeye ni rafiki mzuri wa nesi anayeishi katika ujirani huko. Wanakuja pale juu. Alikuwa anazidi kuwa mbaya. Alikuwa hivyo kwa miaka minane hivi.

37 Na kwa hiyo alikuja hivi majuzi, naye akasema. . . Nikamwambia, nikasema, “Dada, jambo pekee ninalojua, ya kwamba, kuna sababu mahali fulani. Si—sijui ni nini.” Nikasema, “Mimi. . . Ikiwa unaweza kuja.”

38 Akasema, “Nimeombewa; mchungaji wangu.” Na akasema, “Mchungaji wangu alinituma hapa, akasema, ‘Nenda ukamwone Ndugu Billy uone anachosema.’”

39 Naam, nikasema, “Naam, sijui—sijui, dada,” nikasema, “Mimi ni kama mchungaji wako.” Nikasema, “Je, umeungama dhambi zako zote?”

“Kila kitu.”

40 Mwalimu wa shule ya Jumapili, ana darasa kubwa na anafanya kazi nzuri. Lakini hiyo tu ilining’inia juu yake. Vema, si—sikujua la kufanya. Unaweza kuwazia tu jinsi ningehisi. Si—sikujua tu la kufanya.

41 Tukampeleka chumbani. Nikasema, “Vema, njoo huku.” Wakati watu walipokuja, tuliacha tu kila kitu. Nikampeleka chumbani. Nikaketi chini na kuanza kuzungumza juu ya nasaba na kuhusu mwanzo, asili ya wakati na kila kitu, na kumwangalia. Ilikuwa asubuhi hiyo hiyo. Mungu yuko sikuzote katika wakati muhimu, unajua. Na baada ya kitambo kidogo, nikatazama nje, likaja ono likienda juu. Nikaona gari likienda kwa kasi.

42 Nikasema, “Hali yako ina uhusiano fulani na gari.”

Akasema, “Hapana, sikuwahi kuwa kwenye ajali.”

43 Nikasema, “Keti tu kwa unyenyekevu.” Nikasema, “Ninakuona kwenye gari. Unakaribia kugongwa na garimoshi.”

Yeye, aliruka. Akasema, “Loo!”

44 Nikasema, “Ndiyo, na huko na mume wako. Uko na mwanaume mwingine. Mume wako yuko ng’ambo vitani, wakati huo.” Nikaendelea na kuanza kulishusha. Nikasema, “Mambo uliyofanya, mambo ya utovu wa uadilifu! Ulimwambia kuhusu baadhi yake, lakini hukumwambia kuhusu yote.” Naye akaanza

kupiga kelele, akiwa ameshika uso wake namna *hiyo*. Nikasema, "Ulikuwa ufanyiwe upasuaji muda si mrefu uliopita, pia, kwa findo lako, nawe uliogopa kunywa nusukaputi, ukiogopa ungeweza kutaja hilo, chini." Alilia tu kwa nguvu na kuanguka sakafuni.

Akasema, "Hiyo ni kweli."

Nikasema, "Unawezaje kufika popote ukiwa na hiyo ikining'inia?"

Akasema, "Nilimwomba Mungu anisamehe."

45 Nikasema, "Hukumtenda Mungu dhambi. Ulitenda dhambi dhidi ya mumeo na nadhiri." Nikasema, "Wewe rudi na urekebishe hilo, kisha uje. Ninaweza kumdhibiti huyo pepo basi, unaona."

46 Nami nikasema, "Jambo lingine, mume wako," nilielezea jinsi anavyofanana, sikuwahi kumwona maishani mwangu, nikasema, "ana jambo lilo hilo la kukiri kwako." Nikasema, "Sasa, ikiwa huamini, mpigie simu na umwambie akutane nawe." Aliingia na kumpigia simu. Walikutana barabarani.

47 Na hawa hapa wanarudi, machozi yakitiririka mashavuni mwao, wasameheane. Yule pepo akamwacha, na hapo akawa huru. Unaona?

48 Sasa, huenda nilipiga mayowe na kupiga makelele juu ya huyo pepo, na kukemea na chochote kile, na hawakuwa wamewahi kuondoka mpaka hilo liliposahihishwa. Unaona? Unaona, lazima ujue chanzo kabla ya kuweza kupata tiba.

49 Unaenda kwa daktari, unasema, "Nina maumivu ya kichwa." Vema, anaweza kukupa aspirini. Vema, ingerudi. Labda una shida ya tumbo inasababisha maumivu ya kichwa. Labda una maambukizi mahali fulani ambayo yanasababisha homa, kukufanya uwe na maumivu ya kichwa, kitu kingine. Huna budi kurudi, daktari huyo hana budi kuchunguza ugonjwa huo hadi apate kilipo chanzo chake, halafu unaondoa chanzo chake.

50 Kama tu shimo kwenye ndoo, ikiwa unamimina maji ndani, maji yanaendelea kuvuja. Afadhali uzibe shimo hilo, kwanza, unaona. Na hiyo ni . . .

51 Sasa hapo ndipo nilipolala. Nifanye nini? Sasa jambo kuu katika mkutano wangu, lilikuwa hili, huombewi kwa ajili yake. Na nilikuwa nimeomba na kuwaombea wote, lakini wanasema, "Vema, ikiwa ungenigusa tu na utafanya *hivi*," na wao—wanaona mambo hayo yakitendeka.

52 Na ni kweli, Biblia ilisema, "Wanaweka mikono juu ya wagonjwa, nao wanapona." Ndipo unapoanza hilo, nimejaribu hilo, na kuwamulika kwenye mstari, nikaweka mikono juu yao. Lakini kama wao, maisha yao hayajachanganuliwa na Roho Mtakatifu, ili kujua kama kuna kitu chochote mle, hawajisikii

kuwa wameombewa. Huyu hapa katibu wangu ameketi hapa, na mambo mengine ambayo wajua, anapata hizo barua. Hiyo si ni kweli? Wanafikiri tu hawako.

53 Sasa hapo ninapingana na kitu. Na mimi—mimi ninaamini kama ningeweza labda kuhubiri; nami si mhubiri sana, lakini kama ningeweza kuwafanya watu waone ya kwamba hawana budi kujisafisha kabisa na Mungu, basi naamini ningekuwa na mamlaka, kwa Yesu Kristo, kuvunja nguvu za pepo yeyote aliyepo.

54 Petro na Yohana walipopitia kwenye lango liitwalo Zuri, hawakumwuliza kamwe mtu huyo kama alikuwa mwaminio, ama alikuwa nini, ama chochote kile kuhusu jambo hilo. Petro alisema, "Fedha na dhahabu sina, lakini nilicho nacho nitakupa." Kasema, "Katika Jina la Yesu Kristo wa Nazareti, simama na utembee." Akamnyanyua, na kumshikilia pale mpaka mifupa yake ya kifundo cha mguu ilipopata nguvu, na akaenda zake, akitembea.

55 Sasa kuna kitu hapo ndani ambacho ninasomea. Nami nataka uniombee. Vema, utafanya hivyo, kuomba tu? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Mungu awabariki.

56 Fungua, Mwanzo 22 sasa. Nitasoma baadhi, kwa ajili ya somo, kabla ya ibada ya maombi. Vema, tutaanza pamoja kuhusu . . . Wacha tuzungumze juu yake kidogo.

57 Nitakuambia tutafanya nini. Ninataka uingie katika Warumi 4, pia. Nitafundisha kidogo kuhusu imani. Hiyo ndiyo sote tunaihitaji sana. Sivyo? Imani siyo . . . siyo ushahidi tu; ni bayana. Imani yenyewe ni bayana na ushahidi wa mambo ambayo hisia za mwili hazitatangaza. Na nilifikiri, labda, katika kufundisha hili, ingekuwa—ingekuza imani yako, unaona, ifikishe kwenye kiwango ambapo Mungu anaweza kuingia ndani yako na kukubariki.

58 Sasa hebu tuanze kusoma yapata aya ya 8 ya mlango wa 22. Inashughulika na Ibrahimu. Naye aliitwa kwanza Abramu; na kisha akapokea jina lake la kuhani, au jina lake la baba; ambalo, ambalo lilikuwa *Ibrahimu*, ambalo linamaanisha, "baba wa taifa." Sasa sikilizeni:

> *Ibrahimu akazitwaa kuni za hiyo sadaka ya kuteketezwa, akamtwika Isaka mwanawe; akatwaa moto na kisu mkononi mwake; wakaenda wote wawili pamoja.*

59 Ni tukio la ajabu jinsi gani hapa, huko nyuma, miaka elfu moja na mia nane sabini na miwili kabla ya kuja kwa Bwana, Mungu akionyesha kivuli sasa, akizungumza, akijiandaa kufanya m—mfano. Naye, Ibrahimu, alikuwa mzee, mwenye umri wa miaka tisini, na Sara, ama Ibrahimu alikuwa na mia na Sara alikuwa na tisini. Hiyo ni kama miaka arobaini baada ya kukoma

hedhi, kwa hiyo uhai ndani yake ulikuwa umekufa. Na uhai ndani ya Ibrahimu ulikuwa umekufa, mzee katika umri huo.

60 Mungu akamtokea alipokuwa na umri wa miaka tisini na kenda, akasema, "Ibrahimu, tembea mbele Yangu na uwe mkamilifu." Hebu fikiria, katika umri wa miaka mia moja! Naye akamwambia kile ambacho kingetukia. Kasema, "Mataifa yote yatabarikiwa ndani yako, kwa sababu wewe unakwenda . . . Nitakupa mwana kwa Sara." Sasa wazia, umri wa miaka mia moja! Na ndipo Biblia ilisema jambo hilo.

61 Ibrahimu, unajua jinsi alivyoto- . . . akatoa dhabihu yake, na kuwazuia ndege wasiingie humo mpaka jua lilipotua; na jinsi giza lilivyoingia, na Roho wa Mungu akashuka na kuzungumza naye. Naye Ibrahimu alimwamini Mungu.

62 Sasa nataka kushughulika na somo hilo, *Kumwamini Mungu*, ama, kuliamini Neno Lake.

63 Sasa Ibrahimu hakuwa na wingu kubwa la mashahidi kama tulio nao leo hii, kwa maana Ibrahimu mwenyewe alikuwa Mkaldayo, na hata hivyo ni baba wa Wayahudi. Lakini alikuwa Mkaldayo kutoka mji wa Uru. Naye aliitwa kutoka miongoni mwa watu wake, kutembea katika nchi ya kigeni.

64 Jinsi hiyo inavyofananisha matembezi ya Mkristo vizuri sana leo hii, kwamba inatupasa tutoke kutoka kwa washirika wetu wa ulimwengu, kutembea katika nchi ngeni, au ngeni kwa—kwa nchi ya kwanza tuliyotembelea. Na Nchi tunayoiita leo, ni kutembea katika njia ya Kikristo, tutembee pamoja na Kristo, tujitenge na mambo ya ulimwengu.

65 Naye alifanya hivyo kwa imani, na akakaa ugenini katika nchi ya kigeni, bila hata kujua alikokuwa akienda. Jambo pekee, Mungu alisema, "Toka, Ibrahimu, uende katika nchi," naye alikuwa akiutazamia Mji ambao Mjenzi na Mbuni Wake alikuwa Mungu.

66 Sasa kama hilo ndilo tungerejelea katika maisha ya kawaida, ingekuwa, ningesema *silika*, ungeiita kwa kawaida, lakini tunaiita "miongozo ya Roho Mtakatifu." Mungu alimwita atoke miongoni mwa watu wake, kutoka katika nchi, nchi ya wenyeji wake, kutoka kwa watu wake. Naye aliishi katika nchi ngeni, akikiri ya kwamba yeye alikuwa msafiri na mgeni, akitafuta Mji, akitafuta Mji. Loo, jamani, jinsi hiyo ingali inashuka kupitia kwa watoto Wake, tabia hiyo ya kuutafuta Mji ambao Mjenzi na Mbuni Wake ni Mungu! Na Mungu akambariki.

67 Ndipo alipokuwa amezeeka sana, Yeye alisema, "Sasa, Ibrahimu, ulitembea mbele Yangu, ukiwa mkamilifu," na jinsi ambavyo angembariki na kumzidisha. Sasa, kama tuliangalia upande wa kawaida, mbona, haikuwezekana kwake kupata mtoto huyu kwa Sara. Kwa nini, rasilimali zote za maisha zimekwisha. Sara ana umri wa miaka tisini; Ibrahimu mia moja.

68 Mbona, kama ungemwambia jambo hilo daktari leo; m—mwanamume mwenye umri wa miaka mia moja, mke wake akiwa na tisini, mlikuwa mzae mtoto. Mbona, unajua wangefanya nini? Wangekufungia katika wodi ya wendawazimu mahali fulani, wakisema, "Mbona, yule jamaa mkongwe na bikizee amechanganyikiwa kidogo *hapa* mahali fulani." Lakini huangalii hali. Unaangalia ahadi. Unaona? Ukianza kutafuta . . .

69 Sasa hiyo ni vile vile kuhusu labda mama huyo katika kiti cha magurudumu hapa, ama baadhi yenu hapo mlio na kansa. Da—daktari anasema, "Wewe, huwezi kupona." Sasa ikiwa unaamini hivyo, basi huwezi kupona. Lakini huna budi kuangalia ahadi ya Kiungu.

70 Mzee. . . waliitwa mahali pake, akasema, "Ndugu, njoo uombee mtoto wangu, ana dondakoo jeusi na limetulia moyoni. Na picha ya moyo inaonyesha ya kwamba moyo umeanguka nyuma kabisa, na umekwisha."

71 Vema, hawangeturuhusu tuingie ili kumwombea mtoto huyo. Lakini alipofika mle ndani, mbona, loo, yule mkufunzi, daktari, "Hapana, bwana! Hapana, bwana! Huwezi kufanya hivyo. Una watoto wako mwenyewe; huwezi kufanya hivyo."

72 Lakini hata hivyo, kumwamini Mungu, kushawishi. Mtu huyo alikuwa Mkatoliki. Kasema, "Sasa, mbona, kama mgonjwa alikuwa anakufa, na kasisi alikuwa hapa kumfanyia taratibu za ibada za mwisho, ungemruhusu aingie?"

"Loo, hana watoto."

73 "Na sasa hilo silo—hilo silo swali. Hili ni takatifu tu kama taratibu za ibada za mwisho, unaona, za kanisa."

"Vema."

74 Hatimaye nikiingia ndani na kupiga magoti kando ya mtoto mchanga, na kuomba tu maombi rahisi, mafupi; nikaweka mikono juu ya mtoto huyo, nikasema, "Bwana Mungu wa Mbingu na nchi, aliyeumba kila kitu, ulitupa uwezo wa Kiungu ili kuvunja nguvu za Shetani, juu ya maisha haya. Katika Jina la Yesu Kristo, Shetani toka ndani ya mtoto huyu. Ataishi." Nikageuka.

75 Baba huyo, "Asante, Bwana! Asante!" Mama nao wanaanza kucheka na kuendelea.

76 Muuguzi mdogo alikasirika. Akasema, "Sema, unajua jinsi . . . " Akasema, "Ni sawa kuwa na imani, lakini mtoto huyo anakufa." Kasema, "Unawezaje kutenda bila kujali kuhusu hilo? Kwa nini," kasema, "ulimwelewa daktari vibaya." Akasema, "Daktari alisema mtoto huyo anakufa. Amekuwa hana fahamu sasa kwa zaidi ya siku moja." Akasema, "Hukumwelewa daktari."

77 Mzee huyo akasema, "Hapana, sikuele-. . . kutokumwelewa daktari." Akasema, "Nilisikia alichosema; akasema, 'Mtoto huyu anakufa.'"

78 Akasema, "Mbona, lakini, unaona, wakati picha hii ya moyo inapoonyesha kwamba moyo huo uko katika hali hiyo," akasema, "haijawahi kuinuka tena katika historia yote." Akasema, "Ni sawa kuwa na imani, lakini," kasema, "ha—haiwezi. Imani haiwezi kufanya lolote sasa." Unaona?

79 Mzee huyo, kwa kidole kilichotulia, akamtazama nesi na kusema, "Mama, unaangalia hiyo chati. Ninaangalia ahadi ya Kiungu."

80 Mvulana huyo hata ameoa sasa. Vema. Alilala namna hiyo kwa yapata saa ishirini na nne, akalala, na mara moja moyo huo ukaanza kuinuka. Hapo ikaondoka. Unaona?

81 Ahadi ya Kiungu inapotolewa, Mungu yuko chini ya kiapo na wajibu tu wa kushughulikia ahadi zake zozote. Na ninii Yake, ninii . . . Mungu hana thamani zaidi ya Neno Lake lilivyo. Ikiwa Neno hilo halifanyi kazi, basi Mungu hafanyi kazi. *Huyo* ni Mungu. Je, unaamini hivyo? Ni Mungu. Biblia ilisema, "Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwako pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Na mimi sina thamani zaidi ya neno langu, na wewe huna thamani zaidi ya neno lako.

82 Ikiwa ningalikuwa na konzi ya ngano hapa mkononi mwangu, na kuiweka juu ya dawati hili, isingekuwa chochote ila ngano iliyolala pale. Bali panda hiyo ngano ardhini, nayo itazaa labda debe moja ya ngano. Unaona? Lakini, chembechembe ya uhai, hiyo iko kwenye ngano. Lakini ngano haina budi kuanguka ardhini na kufa, Yesu alisema, ama Paulo, naamini, huyo alisema. "Chembe ya ngano isipoanguka ardhini na kufa, hubaki peke yake." Unaona?

83 Na halafu *Huyu* ni Mungu, Neno Lake. Na Neno hilo linapotia nanga chini mo—moyoni! Loo, kama ningeweza tu kukufanya uione! Neno hilo linapotia nanga pale, li—litazaa kile tu lilichosema. Itafanya tu . . . Ni Mungu; inabidi.

84 Lakini ukisema tu, "Vema, najua Neno lipo; naam, hiyo ni kweli," wanakuwekea tu mikono, naam, Hilo—Hilo litakuwa limelala. Hiyo ni kweli, halitasonga, kwa sababu . . . "Loo, mimi, nilisoma Biblia."

85 Lakini mpaka uweze kutia nanga Hiyo, na kusema, "Ndiyo, Bwana, hiyo ni kwa ajili yangu," basi jambo fulani litatokea. Inabidi litokee. Mpaka hapo, ni Neno lililoandikwa tu. Hiyo ni kweli. Lakini wakati limetiwa nanga!

86 Sasa, Ibrahimu, hakuutazama mwili wake. Kasema, "Vema, Bwana, tutapata mtoto." Moja kwa moja tungeweza kuendelea kwa saa nyingi, kwenye hili, lakini hatutaki kuchukua muda

mwingi sana. Sasa anafika mahali ambapo mtoto Isaka anazaliwa.

87 Na hapa anatoka, baada ya kumpokea. Na pengine tu... Ibrahimu labda alikuwa na umri wa miaka mia moja na ishirini, labda, wakati huu, umri wa miaka mia moja na kumi na tano, ishirini. Mtoto Isaka pengine umri wa miaka kumi na mitano, kumi na minane. Na Mungu akasema, "Sasa, Ibrahimu," kasema, "Nataka umpandishe mvulana huyo juu mlimani kule, na umtoe dhabihu." Sasa baada ya kumpokea, alimwahidi "baba wa mataifa," na hapa sasa mzao pekee aliye naye, alisema, "Mchukue na umharibu." Angalia mara mbili. Loo, jamani! Unaona? "Sasa, ninajua ulikuwa mzee, na uliniamini Mimi, nami nikakupa mvulana huyu. Na sasa una—una wazo hapa, sasa, ahadi itatimizwa kwa sababu umepata mvulana. Lakini sasa nataka umchukue huyo mvulana na umwue."

88 Vema, sasa, vipi ikiwa Ibrahimu atasema, "Basi, Bwana, sasa angalia, ninataka kukuuliza jambo fulani. Mimi hapa, labda umri wa miaka mia moja na ishirini, nami nikampokea mvulana huyu. Na maskini Sara hawezi kuzunguka, yeye ni mzee sana, na—naye ameingia makunyanzi na ametoweka, karibu. Na mimi hapa, mzee, lazima niegemee kwenye fimbo, na kutembea hivi," ninatembea kwa shida, labda. "Na mimi ni mzee sana, na—na mvulana huyu ni ki—kijana hapa. Ninaona kile ulichofanya, lakini, je, unamaanisha nimwue? Kwanza, ita—itaurarua moyo wangu kabisa. Na, basi, nitakuwaje baba wa mataifa, Nawe unaenda kumwua?"

89 Lakini Ibrahimu hakusitasita. Alisema, "Ndiyo, Bwana!" Anamchukua mvulana, hawa hapa wanaenda. Hakujua jinsi gani. Haikuwa kazi yake kuhoji. Alitii.

90 Mwanamke hapa anaweza kusema, "Je, nitatembeaje?" Labda umekuwa kilema kwa muda mrefu; sijui. Labda mtu mwingine angesema, "Vema, daktari aliniambia nisingeweza kuishi, Ndugu Branham. Nitakufa." Hilo silo tunalozungumzia. Hilo ni jambo la kawaida, unaona. Ukiangalia lolote la hayo, hutaishi kamwe.

91 Bali huna budi kutazama ahadi ambayo Mungu alitoa, na *Hiyo* ndiyo ahadi. Unaona, ndani yako!

92 Huku nje ni dhambi. Je, ulijua hilo? Unajua mwili wako ni dhambi? Hiyo ndiyo sababu usijaribu kuukamilisha mwili huo, ni dhambi. Je, ulijua hilo? Huo "ulizaliwa katika dhambi, ukaumbwa katika uovu, ukaja ulimwenguni ukisema uongo."

93 Na nafsi hiyo ni vivyo hivyo mpaka nafsi ilipokufa na kisha kuzaliwa mara ya pili na Mungu, basi nafsi hiyo haiwezi kufa. "Nafsi itendayo dhambi itakufa." "Bali yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa milele," basi kuna Uhai usioweza kufa unaoishi katika mwili huo. Sasa, hiyo ni kama kijito kinachotoka

Mbinguni, kama kiini ndani ya mwanadamu. Sasa, hiyo ndiyo sehemu ambayo ni ya kiungu, inayouendesha mwili huu.

94 Lakini kabla mwili huu haujaweza kukamilishwa, Roho atauleta kwa utiifu kwa Mungu, kukufanya wewe. Itapiga vita kila wakati, mara kwa mara. Paulo alisema! Hatutapata zaidi ya yeye. Unaona? Paulo alisema, "Ninapotaka kutenda mema, basi uovu uko karibu nami, unaona." Na hivyo ni vita vya kudumu, mwili dhidi ya Roho.

95 Na hapa unaenda, ukiangalia mwili, "Daktari alisema, na ninaamini..." Angalia ni dhambi jinsi gani! Basi, huwezi kumtumikia Mungu.

96 Unapaswa kutupa kando hisi zako. Mungu hakukupa hizo hisi ili umtumainie nazo. Mungu alikupa Roho Wake kukuamini...mwamini Yeye. Hisi yako ni kuwasiliana tu; kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Lakini kwako, wewe mwenyewe, ndiyo roho hiyo inayoishi ndani yako. Na wakati huo umefanywa upya na mtu wa kale akafa, na mtu mpya kuzaliwa mara ya pili, hiyo ni sehemu ya Mungu; basi unakuwa mwana wa Mungu, mzao wa Muumba. Ndipo unaweza kuamini mambo yasiyowezekana, kwa sababu umeundwa na Mungu atendaye miujiza. Wewe ni sehemu Yake.

97 Ingekuwa kawaida kwangu ku—kunywa pombe; baba yangu alikunywa. Ingekuwa kawaida kwangu kutumia tumbaku; baba yangu alifanya, kizazi changu nyuma yangu kilifanya hivyo. Wengine walisema, "Kwa nini hukuwahi kuvuta sigara au kunywa?"

98 Vema, nilipokuwa tu mvulana, kabla sijaanza, Roho Mtakatifu alishuka, akasema, "Usifanye hivyo!" Huo hapo uongofu, unaona, hapo mwanzo.

99 Na hata huko nyuma kabisa kabla ya hapo, asubuhi nilipozaliwa, wakati Malaika wa Mungu aliposimama pale nilipokuwa, mbegu hiyo ilipokuwa ardhini ilibadilishwa kutoka kwa gugu.

100 Je, huoni ninachomaanisha? Unaelewa ninachomaanisha? Kisha ndani mle kuna roho, na kutoka huko kuna Uzima wako usiopatikana na mauti. Halafu, "Mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu hatendi dhambi." Unapata Maandiko sawasawa basi. Kama yeye, kama... "Mwabudu akiisha kusafishwa mara moja hana tena tamaa ya dhambi, au hajioni tena kuwa mwenye dhambi." Katika Agano la Kale, mwabudu aliingia na kutoa dhabihu yake, akarudi nje akiwa na nia ile ile ya kutenda dhambi. Lakini hapa, hii hapa, ipate, Waebrania ilisema, "Wakati mwabudu, katika hali hii, yeye awekaye mikono yake juu ya kichwa cha Mwana wa Mungu, na dhambi zake zinasafishwa kwa Nguvu za Mungu zitakasazo, hakuna tena tamaa ndani yake ya dhambi." Loo, hapo ndipo Uzima ulipo! Basi, hilo linakufanya uwe mzao wa Yehova.

101 Na Shetani hawezi kuniumiza basi bila kumuumiza Baba yangu. Huwezi kumuumiza yule msichana mdogo pale bila kuniumiza, nitakuambia hilo; siwezi kuwaumiza watoto wako bila kukuumiza. Na, basi, “Hataki mtu yeyote aangamie au kuteseka.”

102 Lakini, sasa, kabla ya mwili huu hapa, kabla mwili haujakamilika, hauna budi kufa kama vile nafsi ilivyokufa.

103 Mungu hakuwahi kuwa na mapenzi Yake makamilifu kwa wanawake na wanaume kuleta watoto duniani. Je, ulijua hilo? Mungu alimfanya mwanadamu, Mwenyewe, kutoka katika mavumbi ya nchi. Baada ya kuanguka. . .Sasa sitabishana kuhusu hilo, kwa sababu mnajua nina maoni ya kuchekesha sana juu yake. Lakini, baada ya kuanguka, basi mwanamke alileta watoto duniani. Mungu akamwambia, “Kwa sababu uliutoa Uhai kutoka duniani, huna budi kuuleta duniani.” Tazama yalikuwa maisha ya namna gani; baada ya kujuana kimwili, shauku, kimwili.

104 Lakini basi mwili huo unapokufa na kurudi ardhini, mavumbi ya ardhi; basi Mungu ataitoa roho isiyoweza kufa kutoka kwake, hadi kwenye Ufalme wa Mungu, au kwenye Kiti Chake cha Enzi, paradiso. Na halafu kwenye Kuja kwa Yesu mara ya pili, mama yangu aliyeketi pale na baba yangu ambaye ametuacha hatalazimika kuupa huu mwili mwingine, lakini Mungu atafinyanga mmoja ulio mkamilifu na usiopatikana na mauti, na usioweza kufa.

105 Sasa Ibrahimu anamchukua Isaka, na wanaanza kuelekea mlimani. Sasa kifungu cha 9.

> *Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu, Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kisha akamfunga Isaka mwanawe, akamweka juu ya madhabahu, juu ya zile kuni.*

106 Sasa kabla tu ya kuja, ninaweza kuwaona wakija; hakumwambia Sara walipokuwa wanaenda, maana angalipiga mayowe. Ninaamini kwamba ilikuwa imani ya Ibrahimu iliyofanya mwujiza katika tumbo la uzazi la Sara; kwa sababu alitilia shaka, hata akacheka wakati—wakati iliposema hivyo. Ilikuwa imani ya Ibrahimu.

107 Kwa hivyo basi hiyo ndiyo sababu, alisema, “Kuomba kwa imani kutamwokoa mgonjwa yule,” maombi ya mtu binafsi. “Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana akiomba kwa bidii.” Loo, laiti ungalijua ya kwamba, mkononi mwako, Kristo alitupa mamlaka, kwa Jina Lake, kwa kuwa Wakristo, silaha yenye nguvu kuliko zote ambayo ulimwengu umewahi kujua. Maombi, hata hubadilisha kila kitu. Yatabadilisha nia ya Mungu. Yalifanya hivyo. Baada ya kifo kutamkwa kwa mtu, aliomba; Mungu alimwambia nabii, “Rudi umwambie nimemsikia.” Tazama hapo, maombi, shikilia!

108 Billy Graham aliulizwa, hivi majuzi. Mattsson-Boze leo yuko kule akipeleka kitabu changu kwa Billy Graham, kwenye mahojiano. Lakini, na wananitaka nimfuate, kule Washington sasa, katika jumba hilo kubwa la mikutano. Tunaweza kuipata. Lakini sasa je, ni mapenzi ya Baba?

109 Walituma jana usiku, kuja Wa-. . .au usiku kabla ya jana, kuja Seattle, tuna mkutano mkubwa unaoendelea kule, naye Kapteni Al Farrar na hao wote wanataka kuja huko sasa, kwa ajili yangu, kuja. Wana mkutano wa Injili, wanautaka. Lakini je, ni mapenzi ya Baba? Hilo ndilo jambo linalofuata.

110 Akaniita, jumba la mikutano, bila malipo, huko Baltimore, huketi watu elfu kumi, haikubidi kulipia hata senti moja. Wahudumu mia tano na majina yao kwenye karatasi, kule nyumbani sasa, "Tutafadhili, asilimia mia moja. Sote tuko katika maombi, kila mahali."

111 "Sasa, Baba, unataka niende wapi?" Hiyo inafuata. "Niambie sasa, na nitaenda." Unaona? Hiyo hapo.

Billy akasema, "Unajua ninaruhusia nini mafanikio yangu?"

Kasema, "Sina fununu."

112 Akasema, "Ninafanya mikutano midogo midogo." Alisikia juu ya mikutano hii. Alitoka nje katika hema dogo, alikuwa huko nje Los Angeles, akifanya tu mkutano mdogo. Na wote wa Chuo cha Northwestern waliangukia kufunga na kuomba. Naye Mungu akateremsha kama waandishi wa habari kumi na watano, na akaleta mkutano wake, nao ukasambaa kote katika taifa.

113 Nilipoanza na madai haya hapa, nililiambia kanisa langu, "Dumuni mkiinamisha uso wenu na mwombe." Mungu akaanza kutenda kazi. Jambo la kwanza unajua, nilisikia simu zikitoka Afrika, kutoka duniani kote. Iliingiaje huko? Sijui. Maombi yalipanda.

Omba! Amini unapoomba. Jambo ndilo hilo. Amini!

114 Ibrahimu, alipokuwa mzee, aliamini. Na Mungu akamwambia aende, naye akatii. Na katika safari yake ya kutoka, ninaweza kumwona akiwachukua watumishi na maskini nyumbu, nao wanaanza kuufikia mlima wa Mungu. Loo, ninapenda tu hili. Sikilizeni hili. Akamwambia mtumishi wake, akasema, "Wewe kaa hapa tunapokwenda kule, na mimi na mvulana tutarudi." Loo, loo, jamani! Samahani, hisia zangu huniacha wakati mwingine. "Mimi na kijana tutarudi." ("Vipi? Sijui. Ninaenda huko kumwua.") Sasa wakati yeye. . .alijua, kwa njia fulani, kwa namna fulani, angerudi, na hapa alikuwa na kisu kikiwa kimechomekwa kwenye mshipi wake.

115 Naye akaziweka kuni mabegani mwa Isaka. Isaka akapanda kilima, akiongozwa na Ibrahimu. Mfano mzuri! Mwanawe wa pekee, akimpeleka kilimani. Na madhabahu ile ile aliyomlaza

mwanawe juu yake, aliipandisha kilimani ameibeba mgongoni mwake. Mfano wa Mungu akimtuma Mwanawe huko Golgotha, akiwa na msalaba wa mbao mgongoni Mwake, msalaba ule ule aliotundikwa juu yake, na ambapo "Mungu hakumhurumia Mwanawe Mwenyewe."

116 Hapo mtoto Isaka alitazama huku na huku, akasema, "Baba," akasema, "hii hapa madhabahu na mo—moto, lakini," akasema, "iko wapi sadaka?"

Akasema, "Mungu atajipatia Mwenyewe dhabihu."

117 Akamfunga maskini mwanawe wa pekee, akamtupa juu ya madhabahu, akachomoa kile kisu na kuanza kuutoa uhai wake. "Mungu, Wewe ulinipa huyu."

118 Naye alipoanza, akavuta kisu chini, Malaika akamshika mkono, akasema, "Ibrahimu, Ibrahimu, simamisha mkono wako!"

119 Hapo hapo maskini mwana-kondoo, kondoo dume, alilia nyikani, ameshikwa pembe zake kwenye vichaka. Ibrahimu akakimbia haraka, akamshika huyo kondoo dume, akamfungua mwanawe; na mbadala, unaona, na kumchinja huyo kondoo. Kisha a . . .

120 Mungu akanena na Ibrahimu, akasema, "Ibrahimu, najua sasa unanipenda Mimi. Hujanizuilia chochote."

121 Sasa angalia, kwa ajili ya somo ninalotaka, hebu na tulisome katika aya ya 13 na 14.

> *Ibrahimu akainua macho yake, akatazama, na tazama, kondoo dume yuko nyuma yake, amenaswa pembe zake katika kichaka: Ibrahimu akaenda akamtwaa huyo kondoo dume, akamtoa sadaka . . . sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanawe.*

122 Unajua huyo kondoo dume alikuwa nani? Huyo alikuwa ni Kristo; alimtoa Yeye, badala yake.

> *Ibrahimu akapaita mahali hapo Yohova-yire: kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa Bwana itapatikana.*

123 Yehova-yire, ambalo lilikuwa ni Jina la kwanza la Mungu la ukombozi. *Yehova-yire* maana yake "Bwana atatoa dhabihu."

124 Sasa, Yeye alikuwa Yehova-yire, Yeye alikuwa Yehova-rafa, -nisi, na kuendelea namna hiyo. Alikuwa na Majina saba ambatani ya ukombozi. Na badala ya uhai wa mwanadamu, alichukua mwana-kondoo na kumtoa kama dhabihu iliyotolewa, kwamba katika Isaka mataifa yote yatabarikiwa, na kupitia Isaka Kristo alitoka. "Nasi tukiwa wafu katika Kristo, twachukua Uzao wa Ibrahimu, na tu warithi sawasawa na ahadi." Haya basi. Na hiyo inaleta, si katika miili yetu; sisi ni watu wa Mataifa katika miili yetu, tu wenye dhambi katika miili

yetu. Lakini katika nafsi zetu, kuzaliwa mara ya pili na Roho yule yule aliyekuwa juu ya Ibrahimu mwaminifu, tabia hiyo hapo ndani hutufanya tutake kumwamini Mungu, lakini mwili unaogopa. Loo, kama sisi ni wana wa Ibrahimu, na tuwe kama baba Ibrahimu alivyokuwa.

125 Sasa *Yehova-yire*, "Bwana atatoa dhabihu." Alitoa dhabihu.

126 Sasa katika Warumi, mlango wa 4, hebu na tuanzie kwenye kifungu cha 17.

> *(Kama ilivyoandikwa, Nimekuweka kuwa baba wa mataifa mengi,)* . . . mabano . . . *mbele zake yeye aliyemwamini, yaani Mungu, mwenye kuwahuisha wafu, na ayatajaye yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako*.

127 Sasa unaona? Ndipo sisi, kama Wakristo, hatuangalii, kuhisi, kuona, kuonja, kunusa, kusikia, tunapozungumza na Mungu. Tunamwamini Mungu tu; na ilihesabiwa kwa Ibrahimu kuwa haki.

128 Sasa, hisi ni vyombo vya kidunia. Je, unaamini hilo? Sasa, Mungu anaweza kuzidhibiti, nitakubali hilo. Lakini hatujapewa hizo kuwasiliana na Baba yetu wa Mbinguni, kwa sababu Yeye hayuko katika mwili wa mwanadamu. Mungu ni Roho. Nasi tunawasiliana Naye kwa roho, kwa njia ya imani, kwa kuamini. Sasa tukisema mimi—mimi nina ninii . . .

129 Nilipokuwa na nywele yoyote, nilikuwa na nywele zenye mawimbiwimbi kama baba yangu. Baba yangu alikuwa na ma—macho ya karibu, ya kina, ya bluu. Watu wengi husema, "Unafanana na baba yako," au, "unafanana na mama yako." Vema, nina mambo mengi ambayo ni—ambayo ni kama watu wangu. Babu yangu mzee alijenga maskani hapa. Wengine wanasema, "Loo, wewe ni kama tu babu yako. Unafanana na babu yako. Unaongea kama yeye. Una tabia kama yake." Hiyo ni nini? Ni tabia fulani ambayo imepitishwa kwenye kizazi hicho, niliyo nayo hapa.

130 Unafanana na mzazi wako, au jambo fulani kuwahusu. Unamwona msichana mdogo, unasema, "Hivi, hafanani na mama yake? Anafanya tu kama mama yake." Umeona watu wakifanya hivyo.

131 Sasa ikiwa tumezaliwa na Baba yetu wa Mbinguni, Mungu, "Ambaye huita vile visivyokuwako kana kwamba vilikuwako," hapana budi kuwa na kitu kama Hicho ndani yetu. Unaona? Hiyo ndiyo sababu kwamba Mkristo halisi aliyejiweka wakfu, hiyo yote ni kwa ajili ya Mungu, hutazamia kile Mungu alisema badala ya kile unachokiona au kuhisi. Huyo ni mtu wa duniani, bado. Tukienenda katika mwili, hatuwezi kumpendeza Mungu. Tunatembea kumfuata Roho. Unaona?

132 Sasa Mungu amefanya kila kitu, zaidi ya jukumu Lake lilivyokuwa kufanya. Ametuma manabii na makuhani. Alituma—Yeye alimtuma Mwanawe. Alimtuma Roho Mtakatifu. Amefanya kila kitu, na hata akaapa kwa nafsi yake kwamba angefanya mambo haya Mwenyewe.

133 Sasa Mungu anapotajirika na kuingia ndani kabisa *hapa* chini! Unaona, kadri unavyozidi kuingiza Mungu *hapa* ndani, ndivyo utakavyozidi kumwamini Mungu, kwa sababu kuna Yeye zaidi. Na kadiri unavyokuza hili *hapa* chini, ndivyo unavyoweza kumwamini Mungu zaidi. Kama tu mtoto, wakati yeye ni jamaa mdogo, labda hajui mengi sana juu Yake, lakini, anapoendelea kukua, anaanza kupata kumjua Mungu zaidi. Na hapo ndipo roho hii humu ndani inapochukua tabia ya Baba yetu wa Mbinguni, ambaye ni Mungu, kama ninavyochukua tabia ya baba yangu wa kidunia kutoka kwa mzazi wangu wa kidunia.

134 Sasa tazama. Loo, naipenda Hii tu! Sikiliza sasa.

> . . .*Mungu, yule* aliyewahuisha *wafu, ayaitaye yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako*.

135 Unajua nini? Mungu aliiumbaje dunia, dunia hii unayoketi juu yake asubuhi ya leo? Watu hawataki kuisadiki imani. Mungu aliiumbaje dunia? Aliinena. Amina. Unaiona? Alinena, na ulimwengu ukatokea. Na ulimwengu huu, asubuhi ya leo, ni Neno lililonenwa la Mungu, na Yeye aliamini Neno Lake Mwenyewe.

136 Hii hapa! Iangalie! Na kama Mungu, na wewe ni mzao Wake, na Mungu yuko ndani yako, Yeye ataamini Neno Lake Mwenyewe. Ingawa haiwezi kuonekana, kuguswa, kuonja, ama chochote kile, utaamini Hilo. Unaona ninachomaanisha? Kwa maana Mungu, ndani yako, ataamini Neno Lake Mwenyewe. Je, hiyo ni kweli? Halafu huangalii vitu unavyoviona. Unaangalia mambo ambayo Mungu alisema.

137 Mwanadamu hana ushindi mwingi anaposhuka. Najua hili, haswa. Mungu hufanya miujiza kupitia kwa mpasuaji stadi, kupitia dawa za matibabu. Mungu huifanya. Mwanadamu haifanyi. Mungu huifanya. Katika Zaburi 103:3, ilisema, "Mimi ndimi Bwana niponyaye magonjwa yako yote." Hakuna uponyaji uwezao kuja, ila kwa njia ya Mungu.

138 Mtu fulani alisema, "Ibilisi anaweza kuponya." Ibilisi hawezi kuponya; anaweza kutoa madai.

139 Kama mtu anayejaribu kurudi kwa meneja, alisema, "Mbona, Ndugu Branham," kasema, "vema, jamani, Yesu alisema, 'Kutakuwa na wengi watakuja Kwangu katika siku hiyo, na kusema, "Bwana, je, nimetoa pepo kwa Jina Lako?" na kadhalika namna hiyo.' Vema," akasema, "hiyo haimaanishi kuwa wewe ni Mkristo. Alikuwa anazungumzia, 'Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.'"

140 Huyo ndugu akasema, "Lakini ngoja kidogo, hivyo ndivyo, enyi kundi la kikanisa." Akasema, "Mnakosa kuona maana halisi ya Maandiko. Nyinyi hufanya makosa kila wakati moyoni mwenu, 'Mkifundisha Mafundisho yaliyo mapokeo ya mwanadamu.'"

141 Walikosa kumwona huyo kwamba ni Mwana wa Mungu. Walisema, "Yeye ni Beelzebuli." Walikosa kuona Maandiko ambayo yalionyesha waziwazi Yesu kuwa huyo.

142 Akasema, "Enyi wanafiki," kasema, "mnaweza kutambua uso wa anga, lakini hamwezi kutambua ishara za wakati. Kwa maana kama mngaliijua, mngalinijua Mimi na kuijua siku Yangu, mambo ambayo yalipaswa kuwa."

143 Nasi tunaona leo hii ya kwamba Mungu aliahidi, katika siku hizi za mwisho, ya kwamba mambo haya yangetukia. Watu wana shida gani? Wao ni vipofu.

144 Nguvu hizo za ibilisi, hata katika ulimwengu wa kikanisa! "Ulisema, 'Yesu hakusema lolote kamwe.'"

Walisema, "Tunatoa pepo."

145 Yesu alisema, "Sikujua lolote kulihusu." Walikuwa wakisema mambo ambayo hawakuyafanya. Loo, sisi . . .

146 Mtu fulani alisema, dhe—dhehebu fulani la kanisa, akasema, "Hebu mhubiri Branham amponye mmoja, nami nitaponya dazeni moja."

Nikasema, "Ikiwa ningemponya mmoja, ungeweza kuponya dazeni moja."

147 Akasema, "Ikiwa ulikuwa na karama ambayo unasema unayo namna hiyo," kasema, "kwa nini usiende hospitali na kusema, 'Ninyi nyote wagonjwa simameni na mtoke nje'?" Akasema, "Itabidi wote wakutii."

Nikasema, "Je, wewe ni mhubiri wa Injili?"

Akasema, "Naam, bwana."

148 Nikasema, "Nenda hapa chini kwenye klabu ya pombe na useme, 'Ninyi nyote mmeokolewa, tokeni nje.'"

Akasema, "Ningeweza kama wangeniamini."

Nilisema, "Vivyo hivyo na mimi ningeweza."

149 Haya basi, imani katika Neno! Unaona? Huwezi kuokoa mtu yeyote. Na kuhubiri Injili ya wokovu hakukufanyi wewe kuwa mwokozi wa Kiungu, si zaidi ya kuhubiri uponyaji wa Kiungu kunifanya kuwa mponyaji wa Kiungu, bali ni imani katika Neno la Mungu lililonenwa.

150 Nami najua haya, kwamba baadhi yetu tuna imani zaidi kuliko wengine, na wale walio na imani nyingi wanatakiwa kuwaombea hao. Lakini ikiwa huishi namna sahihi ya maisha, afadhali uachane nayo; shetani atayacheka maombi yako. Lakini

unapoishi vyema na kutenda haki, na kutenda haki, na kuwa na imani katika Mungu, Shetani atatetemeka unapozungumza, kwa sababu Mungu aliapa chini ya wajibu Yeye angeshughulikia sala hiyo. Hiyo ni kweli.

151 Sasa sikilizeni. Ibrahimu sasa ni mzee. Loo! Nitaharakisha. Mzee sasa, mwenye umri mkubwa, mwenye umri wa miaka mia moja, Mungu alikuwa amempa mtoto huyu, karibu miaka kumi na sita au kumi na minane baadaye; au labda—labda umri wa miaka mia moja na kumi na minane, ishirini. Akasema, "Sasa mpandishe juu, mwangamize."

152 Naye Ibrahimu hakusita katika ile ahadi. Sikiliza hili. Alikuwa kama Mungu, alikuwa na sehemu ya Mungu ndani yake, kwa maana aliamini. Sikiliza, kifungu cha 18.

> Na *ambaye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa;*. . .(Hakukuwa hata na tumaini lolote kwa hilo, hata hivyo yeye). . .*aliamini kwa matumaini, ili apate kuwa baba wa mataifa mengi; kama ilivyonenwa, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.*

153 Sasa sikilizeni, kifungu cha 19. Vaa jaketi; inua kikombe. Tazama.

> *Na yeye asiyekuwa dhaifu katika imani, hakuuzingatia mwili wake mwenyewe uliokuwa umekufa,*. . .

154 Sasa, kama baba yako, Ibrahimu, ambaye wewe ni mtoto wake, kwa njia ya Kristo, hakuuzingatia mwili wake alipokuwa amekufa, vipi kuhusu wako ulio hai asubuhi ya leo? Unaona ninachomaanisha? Na hiyo ilikuwa kabla Kristo hajaja, hiyo ilikuwa kabla ya Upatanisho wowote kufanywa, hiyo ni kabla ya wingu kubwa la mashahidi kutokea, kabla Roho Mtakatifu hajaja, na Ibrahimu alimwamini Mungu! "Kwa kuwa hakuwa dhaifu katika imani, hakuuzingatia mwili wake mwenyewe." Usizingatie ugonjwa wako. Zingatia kile Mungu alichosema kuhusu hilo.

155 Ikiwa ningezingatia yangu, wakati Mayo Brothers waliponiambia, "umekwisha," ningekuwa nimekwisha. Lakini sikuuzingatia mwili wangu. Sikuuzingatia ugonjwa wangu. Sikuzingatia walichosema. Nilizingatia kile Mungu alichosema.

156 Lakini nilipokuwa kipofu, nikizunguka huku nimevaa miwani, singeweza hata kunyolewa; ningevua miwani yangu kwa kinyozi, na kichwa changu kinatikisika mpaka nikae chini, nimwache akate nywele za mtu mwingine kwa muda, kisha arudi kwenye kiti cha kinyozi na ajaribu kukata zangu. Vipi kama ningeizingatia? Lakini sikuzingatia upofu wa macho yangu, nilipomjua Mungu.

157 Daktari aliponiambia, "Funda moja la chakula kigumu litaondoa uhai wako." Nilipolivuta . . . Mama yangu ameketi pale

kama shahidi. Walikuwa wakinipa maji ya shayiri na maji ya zambarau kavu yaliyochujwa; niliishi kwa hayo kwa mwaka mmoja, karibu hivyo. Wakasema, "Vema, funda moja la chakula kigumu litamwua."

158 Nikaanza kusoma Biblia, na nikampata Mungu, nafsini mwangu. Nilisoma pale ambapo ilisema, "Chochote mtakacho, mwombapo, aminini mtakipokea."

159 Hakujawahi kuwa na maombi yaliyosemwa kwenye meza yetu. Nakumbuka baba akiketi pembeni pale. Nilisema, "Je, tunaweza kuomba?" Mama alitazama na kuanza kulia. Naye baba hakujua la kufanya.

160 Nikasema, "Mungu!" Alikuwa na Biblia juu ya meza. Nikasema, "Kama nikifa, nitakuja Nyumbani, nikikutumaini Wewe. Neno Lako lilisema hivi. Sina budi ama kutafakari kile daktari alichosema, ama kuzingatia ulichosema Wewe. Nimechukua neno lake kwa mwaka mmoja na sina afueni hata kidogo; hali yangu inazidi kuwa mbaya. Sitazingatia alichosema, tena. Ninazingatia ulichosema Wewe." Ndipo nikaomba baraka.

161 Tulikuwa na maharagwe, na ugali wa mahindi, na vitunguu. Nilitoa sahani iliyojaa hizo, nikaanza kula. Tonge la kwanza lililoingia tumboni mwangu, nusura liniue. Ilibidi nishikilie kinywa changu kwa mkono wangu ili kulizuia lisirudi. Nalo liliendelea kurudi, na ningelimeza; linarudi, ningelimeza. Lakini sikulizingatia tumbo langu. Nilizingatia kile ambacho Mungu alisema juu yake, si kile nilichohisi; ilikuwa inanichoma.

162 Nilitoka barabarani, na nilikuwa nikitembea barabarani *hivi,* maji yakitoka kinywani mwangu. Akasema, "Unajisikiaje, Billy?"

Nikasema, "Vizuri sana!"

163 Siku zikapita, wiki zikapita; ningali nikitembea, nikisimama chini shimoni, huku tumbo langu likiwa hivi, nikiwa nimeushika mkono wangu namna *hiyo*. Nikigonga namna *hiyo*; nikiimba, "Loo, jinsi ninavyompenda Yesu!" Naliweka chini, kisha natupa uchafu mwingine ndani; napaza sauti, "Loo, jinsi ninavyompenda Yesu." Nikiteuka tu chakula hicho, nikirudi, nikiwa na kizunguzungu sana nisingeweza kufanya kazi.

Kasema, "Unajisikiaje asubuhi ya leo? Billy, wewe ni mgonjwa?"

Nikasema, "Hapana. Najisikia vizuri sana."

164 Kisha, baadaye niliposhuhudia, mtu fulani akasema, "Ulisema uwongo basi."

165 Nikasema "Hapana, sikusema uwongo. Sikuwa nazungumzia hisia hizi hapa mwilini; zimekufa. Nilimtambua Kristo akitiririka kutoka kwangu." Nikasema, "Nilikuwa nikichukua kile alichosema Yeye, na nikajisikia vizuri sana juu yake."

166 Haya basi. Usizingatie mwili wako mwenyewe. Msiyazingatie magonjwa, maana ni ya ibilisi. Kweli. Zingatia ahadi ya Mungu.

167 Mtu fulani si muda mrefu uliopita alisema, "Sasa, angalia, huwezi kuhubiri uponyaji wa Kiungu katika Upatanisho." Mhubiri mwerevu, Mbaptisti, ambaye alikuwa . . .? . . .

168 Nikasema, "Sasa sitabishana nawe kuhusu Upatanisho, ambao najua huna msingi wa kusimamia; wa kimsingi sana." Nikasema, "Najua huna msingi . . . Hili hapa Andiko moja, kati ya arobaini, litaondoa jambo hilo lote. 'Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu iko juu Yake, kwa kupigwa Kwake sisi tumepona.'" Nikasema, "Je, unalitumia wapi hilo, Kalvari?"

169 Nikasema, "Je, unaamini yale majina saba ya ukombozi, majina ambatani, ni ya Yesu? Kama hakuwa hivyo, wala hakutimiza, na ndani Yake mlikuwa na hayo majina saba ambatani, Yeye hakuwa Yehova-yire. Kuna *Yehova-yire,* 'dhabihu ya Mungu iliyotolewa,' na itabidi ukubali hilo au kusema Yeye hakuwa Mwana wa Mungu. Basi ikiwa Yeye ni Yehova-yire, Yeye ni *Yehova-rafa,* 'mponyaji,' pia. Maana, majina yote saba ambatani, 'ushindi wetu,' 'bendera yetu,' na 'ngao yetu,' na 'kinga yetu,' na 'uponyaji wetu,' na 'wokovu wetu,' 'dhabihu yetu iliyotolewa,' yote yaliwekwa ndani Yake! Na alipokufa pale Kalvari, aliharibu falme; akafufuka, akatupa mikono Yake nje, akasema, 'Imekwisha!' Haleluya! Pepo walitetemeka; kuzimu ilitikisika; ni mfano kwa kila njia. Naye akafufuka asubuhi ya Pasaka, 'Mimi Ndimi niliyekuwa nimekufa na ni hai tena.' Huyo hapo, Yehova-rafa, Yehova-manase. *Yehova-yire,* 'dhabihu ya Mungu iliyotolewa.'" Hangeweza kuwa na neno la kusema.

170 Kisha kule nyuma, kama Yesu alivyosema, "Kama Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa." Na kama kuangaza nuru hiyo ya Mungu kule nyuma, kwa mfano, kuangalia nyoka wa shaba ambaye alikuwa ni mfano . . .

171 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Alisema, "Inabidi nitimize neno langu. Huna budi kufa." Maskini jamaa huyo alitetemeka. Akasema, "Nikupe nini kabla sijakuua?"

Akasema, "Bilauri ya maji."

172 Basi akaenda na kuchukua bilauri ya maji. Naye alikuwa ameishikilia mkononi mwake, na akitetemeka namna *hiyo,* hangeweza kuishikilia. Naye akasema, "Sasa, ngoja kidogo, jinyooshe." Akasema, "Sitakuua au kuondoa uhai wako mpaka unywe maji hayo." Na mtumwa akaitupa chini. Atafanya nini? Ikiwa yeye ni mtu mwadilifu, kama atatimiza neno lake. Asipotimiza neno lake yeye si mtu mwadilifu. Inabidi amwachilie huru, bila kujali sheria za nchi zilisema nini.

173 Na kama Yesu alisema, "Mambo yoyote mtakayo, mwombapo, aminini ya kwamba mtapokea," hana budi kulitimiza. Yeye ni mwenye haki. Upatanisho, ama bila Upatanisho, hilo ni Neno Lake.

174 Mvulana alienda si muda mrefu uliopita kwenye seminari fulani, ili kujifunza mambo mengi sana ambayo hakupaswa kujifunza. Kwa hivyo maskini mama yake aliugua. Mmoja wa majirani zake alikuwa wa kanisa la Full Gospel, walimleta mchungaji nyumbani. Kasema, "Acha nimlete mchungaji hapa na kukuombea." Akasema, "Yeye ni mtu mwema, mwadilifu, na anamwamini Mungu," kasema, "hebu aje akuombee."

Kwa hivyo yeye akasema, "Vema."

175 Daktari asingeweza kufanya chochote kwa ajili yake, kwa hiyo kijana huyo akaja pale, mchungaji, na kumwombea huyo mwanamke mkongwe, na akaweka mikono yake juu yake kulingana na Yakobo, au kulingana na Marko 16. "Wataweka mikono juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Alikuja na kuweka mikono yake juu ya mwanamke huyo. Siku chache, alikuwa ameamka na anaendelea na kazi yake, alikuwa mzima.

176 Mwanaye aliporudi nyumbani kutoka chuoni, mbona, alikuwa na furaha sana, mwajua, naye anamwona mama yake akiwa na furaha sana, akasema, "Umekuwa ukiendeleaje, mama?"

177 Akasema, "Vizuri tu." Akasema, "Loo, mwanangu, nilisahau kukuambia jambo fulani." Akasema, "Ulipokuwa umeondoka miaka hii minne," kasema, "Niliugua. Na, unajua, Bibi *Nanii* hapa ni mfuasi wa lile kanisa la Full Gospel." Akasema, "Mchungaji wake alikuja na kuniwekea mikono kulingana na Marko 16, nami nikapona." Akasema, "Madaktari hawakuweza kunifanyia lolote nilipokuwa na ugonjwa huo." Kasema, "Hivyo ndivyo nilivyopona."

178 Akasema, "Vema, mama, nataka kukujulisha jambo." Akasema, "Bila shaka, huko chuoni, tunajifunza hili." Akasema, "Vifungu tisa vya mwisho vya Marko 16 havijavuviwa." Akasema, "Hilo liliwekwa pale na Vatikani." Akasema, "Hakuna historia inayosema kwamba Neno hilo hapo ndani limevuviwa."

Ndipo maskini mwanamke huyo akasema, "Mungu asifiwe! Mungu asifiwe!"

Akasema, "Una shida gani, mama?"

179 Akasema, "Kama Mungu angeweza kuniponya kwa Maneno hayo 'yasiyovuviwa,' angeweza kufanya nini na Yale ambayo yamevuviwa?" Haya basi. "Kama angeweza kufanya hivyo na Maneno 'yasiyovuviwa,' angefanya nini na Yale yaliyovuviwa?"

180 Wakati kuna ahadi mia sita na kitu zilizoelekezwa kwa Kanisa katika siku za mwisho, kwamba mambo haya yatatukia, na Nguvu Zake zingali zile zile! "Yesu Kristo yeye yule

jana, leo, na hata milele. Chochote unachotamani unapoomba, amini unakipokea. Mkikaa ndani Yangu na Neno Langu ndani yenu, ombeni mtakalo nanyi mtatendewa. Mambo nifanyayo ninyi nanyi mtayafanya; kubwa kuliko hili, niendapo kwa Baba Yangu. Tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari. Popote walipo wawili au watatu wamekusanyika kwa Jina Langu, na kukubaliana juu ya chochote na kuomba, watapokea."

181 Sahau hilo, ndugu. Ni mapenzi ya Mungu kufanya hivyo. Ndiyo, ni Shetani tu anayekuibia. Mwamini Yeye.

> Naye *aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate* kuwa *baba wa mataifa mengi; kama ilivyonenwa, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.*
>
> *Wala yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, hakuuzingatia mwili wake mwenyewe uliokuwa umekufa,. . .*

182 Sio hali, sio kile mtu mwingine alisema, "Vipi kama mtu mwingine alikufa, wakati, una jambo lile lile?" Usiizingatie, unaona.

> *. . .akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia moja, wala. . .hali ya kufa ya tumbo lake Sara:*

183 Alijumuishwa ndani yake. Mungu kamwe hakumpa Sara ahadi; alimpa Ibrahimu ahadi, lakini Sara alijumuishwa. Alitoa ahadi katika Kristo Yesu, nami nilijumuishwa ndani Yake, nanyi pia mlijumuishwa. Unaona?

> *Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini; bali alitiwa nguvu kwa imani, akimtukuza Mungu;*
>
> *Huku akijua hakika ya kuwa, yale aliyoahidi, alikuwa na* uwezo pia *wa kufanya.*
>
> *. . .kwa hiyo ilihesabiwa kwake kuwa haki.*
>
> *Sasa haikuandikwa kwa ajili yake peke yake,. . . haikuhesabiwa* ila *kwake;*
>
> *Bali na kwa ajili yetu sisi mtakaohesabiwa vivyo hivyo, ikiwa tunamwamini yeye aliyemfufua. . .Yesu Bwana wetu kutoka kwa wafu;*
>
> *Ambaye alitolewa kwa ajili ya* kosa *letu, na kufufuka tena kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu.*

184 Loo, ndugu, hiyo tu. . .Ninaweza tu kumpiga ibilisi usoni kwa jambo hilo, kwa siku mia tatu na sitini na tano kwa mwaka, unaona. "Wewe ni mwongo. Hilo hapo Neno; nimepona."

185 Ikiwa mtu atakuja na kuweka juu yako, kama mtu fulani alitoka hapa na kukufanyia jambo fulani, na kukufanya upone, haikutii moyo. Lakini hivi ndivyo ilivyo, yeye aaminiye, "Nimepona sasa."

186 Kama Mungu alishuka na kuniponya hakika, moja kwa moja, kwa mwujiza, haingekuwa kubwa kama ingekuwa kama ningeona ahadi ya Mungu na kuiweka moyoni mwangu. Nikisimama hapo, naweza kusema, "Yesu sasa ananiponya, kwa maana nimekubali Neno Lake. Liko moyoni mwangu. Sasa ananiombea mbele za Baba. Nitakuwa mzima." Hicho hapo anachokipenda Mungu. Simama hapo kwenye Neno Lake na useme, "Ni kweli! Ananiponya sasa, kila siku."

187 Huyo alikuwa ni yule mwanamke aliyekuwa na tezi, "Naweza kuona." Ninampa tu kitu cha kufanya. Kwa hiyo. . .?. . .[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .hataki yoyote kabisa. Lakini alikuwa na furaha, akasema, "Loo, tazama, tazama!" Na siku iliyofuata ilikuwa karibu kiasi *hicho*. Kisha siku iliyofuata, karibu kiasi *hicho*. Aliweka yote pamoja, akasema, "Hiyo, *hiyo* haiwezi kukosea." Unaona, haya basi.

188 Eliya alipokuwa amezifunga mbingu, mvua isinyeshe kwa muda wa miaka mitatu, Eliya alifanya hivyo, "mvua isinyeshe miaka mitatu na miezi sita," na alipokiinamisha kichwa chake kati ya maskini magoti yake yaliyokonda. Pengine, kama angekuja kwenye mlango wako asubuhi ya leo, ungemfukuza. Akiwa na manyoya kichwani kama sijui nini, huku amejizungushia kipande kidogo cha ngozi ya kondoo *hivi*, na chupa ya mafuta na fimbo, naye huyu hapa anakuja, kile kichwa chenye upara kiking'ara. Akaketi pale, akaweka magoti yake chini, kichwa chini katikati ya magoti yake, na akaomba, "Mungu, shida imeisha sasa. Israeli imetubu. Njoo, Bwana, uwanyeshee mvua."

189 Kama yule mwanamke hivi majuzi, wakati dhambi imekwisha, nilisema, "Shetani, huwezi kumshika." La, bwana. Ndivyo ilivyo.

190 "Njoo, Bwana. Vema, shida imekwisha." Aliomba mara sita, akarudi chini. Hilo halikumzuia, aliendelea kuomba. Hiyo ni kweli. Kisha baada ya kitambo kidogo, Gehazi anapanda juu, mtumishi wake, anatazama. Naye akarudi, akasema, "Loo, naona wingu dogo karibu ukubwa wa mkono wa mwanadamu."

191 Mbona, anga, mvua haikuwa imenyesha kwa miaka mitatu na miezi sita. Shaba! Shaba hunena juu ya hukumu ya Kiungu, madhabahu ya shaba, hukumu juu ya taifa lililokuwa limemsahau Mungu, anga za shaba. Laiti tungekuwa na wakati wa kuingilia hilo. Lakini, basi, kutokuamini kungalilichukua hilo na kulitupilia mbali, "Vema, ikiwa ni hivyo tu unaweza kunituma!" Ndiyo.

192 Lakini Eliya aliona nini alipoona gurudumu la kwanza kabisa likizunguka? Loo, jamani! Alisema, "Nasikia sauti ya mvua nyingi." Hakuna wingu kubwa kuliko *hilo*, lingefanya nini kulinywesha taifa maji? Kwa nini, ikiwa wingu ni ninii sana. . . Ni joto sana katika anga hizo hata ingekuwa, "wee," iliuvukiza,

mvuke ungeenda *hivyo*. Lakini mara Eliya alipoona ishara ya kwanza, mwenendo mdogo wa kwanza, alisema, "Nasikia sauti ya mvua nyingi," wakati ni wingu wenye ukubwa *huo* tu.

193 Ndugu, naamini, ninii. . .sasa hivi katika dakika hii, kwamba nguvu za Roho Mtakatifu, zilizoko katika chumba hiki, ili kutuliza kila mgonjwa aliyepo, kwamba unaweza kuhisi wingu ukubwa wa mkono wa mtu, akipiga makelele na kupaza sauti, "Nasikia sauti ya uponyaji mkamilifu." Mungu hana budi.

194 Unakataa na kusema, "Vema, sikupata chochote," basi watakufa, mawimbi ya moto ya kuzimu na mashaka yataififisha kutoka nafsini mwako.

195 Lakini unapopata hiyo punje ndogo ya Mbegu, simama juu Yake. Sio kama mwamba wa Gibraltar. Ni kama Mwamba wa Miaka. Simama hapo na utasikia sauti ya mvua nyingi. Wewe ni mtoto wa Mungu. Shetani ameweka mateso hayo juu yako. Na unajua nini? Na Kristo tayari amewaponya kila mmoja wenu.

196 Mwenye dhambi anakuja madhabahuni na kusema, "Ndugu Branham, mimi, naam, nataka uniombee. Na—nataka kuwa mzuri, lakini mimi tu . . . Wewe niombee," kisha unarudi kwenye kiti chako.

197 Usiku unaofuata, ninasema, "Ni wangapi wanataka kuokolewa?" Huyu hapa anasimama. "Unataka kuokoka, kijana?"

"Naam, bwana."

"Kweli, kwa nini usiokolewe?"

"Sijui."

198 Akasema "Wewe tu . . . " Ibilisi amemshikilia mvulana huyo. Ni hayo tu. Anataka kufanya mema, lakini kuna roho, nguvu ambayo haitamruhusu kuwa sahihi.

199 Sasa, haleluya, hiyo hapo! Si ajabu. . .Mungu hataruhusu kamwe mtu wa kweli wa Mungu aseme angeweza kumponya mtu fulani. Kristo alifanya hivyo alipokufa. Nisingeweza kuokoa mtu yeyote, au hakuna mwingine anayeweza kuokoa mtu yeyote, isipokuwa Mungu.

200 Na Mungu hawezi kukuokoa, kwa sababu tayari ameshafanya hivyo. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kuukubali. Tayari imefanywa. Sikuokolewa miaka ishirini iliyopita; niliokolewa miaka elfu moja na mia tisa iliyopita, lakini miaka ishirini iliyopita niliupokea na kuukubali. Kama sivyo, dhambi ya kwanza niliyofanya, Mungu angeniondolea juu ya uso wa nchi; maana Yeye alisema atafanya, Naye hana budi kutimiza ahadi Yake. Niliponywa miaka elfu moja mia tisa iliyopita, lakini sina budi kuukubali.

201 Na kitu pekee ambacho kilinizuia kuokolewa nilipokuwa na umri wa miaka kumi na miwili, kwa sababu roho

fulani alinizunguka, ibilisi, akisema, "Subiri kwa muda zaidi kidogo." Hiyo ndiyo sababu hukuokolewa ulipofikisha umri wa kuwajibika. Roho, uliingia kwenye umati, na hiyo ikaelea juu yako na ikaendelea kuning'inia juu yako. Ulitaka kutenda yaliyo haki. Hakuna mtu ambaye ana akili timamu ila anayetaka kufanya yaliyo haki, lakini kuna kitu hakitakuruhusu kutenda haki. Je, hiyo ni kweli? Huyo ni ibilisi. Haleluya! Kristo alilipa uponyaji wako na wokovu wako.

202 Sasa hii hapa. Jiweke tayari. Aliliamuru Kanisa Lake kuwatoa hao pepo. Haya basi. "Kwa Jina Langu watatoa pepo. Hutamponya mtu yeyote, lakini utamtupa shetani mbali nao ili waweze kukubali uponyaji ambao tayari nimefanya." Hiyo ni kweli.

203 Wahubiri walisimama jukwaani na kuhubiri Injili, pepo wakatawanyika. Mtu huyo alikuja madhabahuni, chini ya sadikisho, kasema, "Ninataka kuokolewa." Yeye kamwe hakumwokoa mtu huyo; alimtoa ibilisi, hiyo ni kweli, ndipo mtu huyo akaokolewa. Alikuja, akakubali wokovu wake.

204 Jambo lile lile kwa uponyaji wa Kiungu. Enyi watu wagonjwa hapa asubuhi ya leo, aminini hilo, na mmezaliwa mara ya pili, na ni wana na binti za Mungu, Kristo tayari amekuponya. Kitu pekee kinachokuzuia kuwa mzima asubuhi ya leo ni roho inayoning'inia juu yako ambayo haitakuruhusu kabisa uende kule na kuamini ahadi ya Mungu ya kwamba amefanya jambo hilo. Hiyo ni kweli.

205 Sasa, hilo ndilo agizo langu. Hicho ndicho Mungu alichonipa, ndicho anachompa kila mhubiri wa Injili atakayeamini, uwezo na mamlaka ya kuivunja roho hiyo. Ninaamini kwa moyo wangu wote kwamba kila nguvu ya pepo iliyo hapa ndani dakika hii tayari imevunjwa. Ninaamini. Ninaamini kuna kila mgonjwa humu ndani sasa hivi anajisikia tofauti sana. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, ninyi mliokuwa wagonjwa. Tazama hapo. Wewe, kuna nini? Huyo shetani amejitenga na wewe. Inabidi ajitenge. "Imani chanzo chake ni kusikia, kusikia Neno." Yesu Kristo alikufa kwa ajili yako.

206 Unaweza kuponywa sasa hivi, ili kutimiza agizo hilo. Ninyi watu ambao ni wagonjwa hapa asubuhi ya leo, ama mmeingia, ama mliingia hapa hivyo; huku Roho huyo akiwa juu yako, huku unapomhisi Roho wa Mungu. . . Inakaribia, loo, samahani, imepita kabisa. Enyi watu wote ambao ni wagonjwa, mliokuwa wagonjwa mlipoingia hapa, nataka mje hapa ili niweze kutimiza agizo langu. Mimi nina wajibu kwa Bwana wangu.

207 Na madai yangu, kama Malaika wa Kiungu alivyonitokea wakati wa kuzaliwa kwangu, na kuniagiza nikiwa na umri wa miaka kumi na miwili, na kunituma hapa miaka michache iliyopita, na kusema mambo haya, na ni jambo lisilopingika

kote ulimwenguni. Mapepo na—na makafiri, na wenye shaka na wakanamungu, na—na wanaukisasa na wakomunisti, na kila kitu kingine, kimeishambulia kwa njia za kusema ilikuwa. Baadhi yao walisema, "Uabudu mizimu." Baadhi yao walisema, "Ni kazi ya shetani." Na yule mwingine akasema, "Ni—ni telepathia ya kiakili." Na kila mara walipoinuka, Mwenyezi Mungu alisimama mbele yangu na kulishinda. Hiyo ni kweli. Ipeleke popote unapotaka, katika taifa lolote utakalo. Kila taifa ambalo nimeingia, kila mji, karibu, imenibidi kupigana na kitu hicho; wanasema, "Ni telepathia ya kiakili."

208 Ningesema, "Mwondoeni kila mtu hapa anayefikiri ni telepathia ya kiakili. Ondoeni kila mtu anayejua chochote kunihusu. Nileteeni mgonjwa."

Kasema, "Ni uabudu mizimu."

209 Nasema, "Basi ikiwa mimi, kwa uabudu mizimu, ninaleta watu kwa Yesu Kristo na kuwashinda pepo, wewe unafanya nini na ulicho nacho? 'Amueni kwa matunda yao,' Yesu alisema, 'mtawajua.' Je, umewahi kumwona mwabudu mizimu akitoa pepo? Kamwe hutaona. Hiyo ni kweli." Nikasema, "Yesu alisema, 'Kwa matunda yao watawatambua.'" Nilisema, "Katika miaka michache iliyopita, kwa neema ya Mungu, nimeleta nafsi mia tatu na hamsini elfu kwa Kristo. Umefanya nini wewe?"

210 Mwanamume mmoja alikutana nami hapa nje na kusema mwanamke fulani alimwambia ya kwamba mimi ni—nilikuwa ni ibilisi, na kazi yangu yote ilifanyika kwa ibilisi. Walijiondoa kanisani hapa, nao wana kundi lililokimbia pamoja nao, na namna hiyo.

211 Nikasema, "Umefanya nini? Nionyeshe tunda. Alianza kule chini, na Mungu akaing'oa. Alisema, 'Kila tawi ambalo ninii yako . . . Baba yetu wa Mbinguni hajapanda litang'olewa.'"

212 Nilipoiweka hiyo maskani kwenye kona, na kupiga magoti hapa juu ya lundo la magugu ya jasi na magugu ya farasi hapa, na hii moja kwa moja juu ya mimbara hii asubuhi ya leo, ilipokuwa kidimbwi, Mungu alisema, "Nitakibariki."

Hawa hapa walisimama manabii wa uongo, wakasema, "Niliona magari yakiingia na kutoka. Nami nikaona mawe yakienda moja kutoka kwa jingine." Hiyo ilikuwa miaka ishirini iliyopita, na leo bado inaendelea, nayo itasonga mbele, maana ilijengwa hapa kwa jasho na machozi ya maombi na ahadi ya Mungu. Itashinda.

"Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, malango ya kuzimu hayatalishinda." Haya basi. Ndiyo, bwana. Usizingatie kile wanachosema. Nimejifunza somo langu la kusikiliza watu ambao hawajui wanazungumzia nini. Ninamsikiliza Mtu mmoja, huyo ni Mwenyezi Mungu. Yesu alisema, "Tangu sasa ombeni kwa Jina Langu, mwombeni Baba katika Jina Langu, nanyi mtapata." Ninaiamini.

213 Wakati mmoja huko Harlingen, Texas. Mimi. . .hiki—hiki ndicho nilichokuwa najaribu kujiepusha nacho; kinachoma moyo wangu. Walikuja kule, nami ninayo katika ninii yangu, la, iko katika kitabu changu kidogo cha kiada, cha jambo fulani. Alisema kuwa nilikuwa. . .FBI walikuwepo kunifichua, kwamba nilikuwa i—i—ibilisi. Na wahudumu, kundi lao kule juu mahali fulani juu ya Houston kule, nitataja jina la mahali hapo kwa dakika moja; akatoa lundo kubwa la vitini na kuvipitisha kote, juu yake, namna hiyo, kwenye jumba la mikutano, na kusema kwamba mimi ni Simoni mchawi, nikitoa pepo kama Simoni mchawi, uchawi.

214 Kwa hivyo usiku huo hapa, kulikuwa na wasichana wawili waliokuwa wameponywa pale, nao wakaja, wakilia na kila kitu, kasema, "Naam, unapaswa. . .nilisema. . .Walisema wanaenda nyumbani, waliogopa. Kasema, 'FBI itakuchukua, Ndugu Branham.' Na msichana huyu aliwekwa katika akili yake timamu ulipoona ono hilo juu yake." Na mimi. . .Akasema, "Ni—nilikosea. Labda nimesababisha shida."

215 Nikasema, "Loo, unaogopa." Nikasema, "Umemwona Mungu Mponyaji, sivyo?" Nikasema, "Mwangalie kama Shujaa. Mwangalie katika vita, uone jinsi alivyo mkuu. Tazama jinsi Mungu alivyo mkuu kama Shujaa katika vita!"

216 Usiku huo nilitoka nje, nikasema, "Kila mtu katika hii, hapa katika kampeni yangu, Bw. Baxter, ndugu yangu, na wale wasichana wawili waliopонywa, na hao wanaohudumu walisema leo ya kwamba umejumuishwa kwao, nataka mtoke nje ya jengo." Wakatoka nje ya jengo. Nikasema, "Sasa, nina kipande cha karatasi hapa ambacho msimamizi wa jumba hilo alitoka nje na akatoa maelfu yao kutoka kwenye magari, akaajiri watoto wadogo wa Meksiko kwenda kuwachukua." Nikasema, "Nina bili ndogo hapa inayosema hapa usiku wa leo kwamba mimi ni Simoni mchawi na nitafichuliwa na FBI hapa usiku wa leo."

217 Nikasema, "Vema, FBI, niko jukwaani katika Jina la Bwana Yesu Kristo; njoni jukwaani sasa mnifichue." Nikasema, "Kama ninafanya jambo lolote nje ya Biblia ya Mwenyezi Mungu, njoni hapa mkanifichue." Nikasema, "Mko wapi?" Maelfu wameketi pale na kila mtu alikuwa analia. Nikasema, "Nasubiri FBI. Kulingana na karatasi yenu hapa, mlikuwa mnifichue usiku wa leo." Hapo hapo nilingoja dakika chache, na nikahisi roho hiyo ikitoka. Nikasema, "Haikuwa FBI. Mimi si mhalifu." Nikasema, "Kila wakati wakala wa FBI alipokuja kwenye mkutano wangu, walipata—waliokolewa. Mkuu wao aliokolewa katika mkutano wangu, Kapteni Al Farrar." Nikasema, na, loo, nikasema, "Hakuna FBI inayofanya kitu kama hicho."

218 Nikasema "Jambo lenyewe, ni wahubiri wawili waliorudi nyuma." Nikaangalia, kikining'inia pale, na kulikuwa na

kitu kikubwa cheusi kikiwa kinaning'inia juu ya wasikilizaji. Nilikiona kikienda juu hivi kwenye roshani ya pili. Nikasema, "Papo hapo, ameketi, mmoja amevaa suti nyeupe, mmoja amevaa suti ya kijivu." Nao wakashuka namna *hiyo*.

219 Nikasema, "Usishuke! Nilifikiri ulikuwa unaenda kunifichua. Unaaonekana kama mtu mwingine." Nikasema, "Nyinyi ni wahubiri kadhaa waliorudi nyuma. Hamna uhusiano wowote nayo." Nami nikasema, "Basi, ikiwa mimi ni Simoni mchawi, na kutoa pepo kwa uchawi, kama msemavyo kuwa ninatoa, na nyinyi ni watakatifu na wenye haki katika Mungu, shukeni mje jukwaani. Ikiwa mimi ni Simoni mchawi, nitaanguka nife. Kama wewe ni Simoni, kama wewe ndiye uliyekosea, utaanguka ufe. Shukeni chini sasa, tutaona ni nani aliye sahihi." Hiyo ni kweli, nikawaweka kwenye changamoto. Waliinamisha vichwa vyao. Nikasema, "Msiinamishe vichwa vyenu hivyo."

220 Nikasema, "Sasa, enyi watu, mnaona ni nani aliye sahihi na ni nani aliye makosani. Wanaogopa." Na hapo wakatoka juu ya pale, haraka sana wakienda. Nikasema, "Loo, naona wanaondoka. Labda wanashuka hapa." Walitoka nje ya jengo haraka walivyoweza, wakishuka kwenye vipandio. Nilisimama pale na kungojea. Nikasema, "Sasa tutaona. Waache waje jukwaani. Acha Mungu aonyeshe nani ndiye nani." Hiyo ni kweli. Nikasema, "Ikiwa mimi ni mwongo, basi Mungu ataonyesha kuwa ni uwongo. Nikiwa sahihi, Mungu daima ataitetea kweli."

221 Kama ilivyokuwa huko Houston wakati mhubiri huyo wa Kibaptisti aliposema kwamba mimi ni pepo, na kadhalika, basi unaona kilichotukia wakati Malaika wa Bwana aliposhuka.

222 Sasa, unajua nini kilitokea? Hatukuwaona tena. Usiku huo Bwana alitupa ushindi pale ambao bado unazungumziwa huko Harlingen. Unaona? "Mimi Bwana, nimeipanda. Nitainywesha maji mchana na usiku, wasije baadhi ya watu kuinyakua kutoka mkononi Mwangu."

Njoni sasa, enyi wavulana, mtafika kwenye piano haraka sana?

223 Hebu wagonjwa, ama walio wagonjwa, waje karibu na madhabahu upesi sana sasa. Tuna takriban dakika kumi hapa, na tutakuweka huru kutoka kwa kila nguvu ya pepo inayokuzunguka, katika Jina la Bwana Yesu. "Ninawapa Jina Langu na mamlaka."

224 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .Nikijaribu hili kwa sababu ninaamini kwamba Mungu ameniweka kufanya hivyo. Ninaiamini. Kama tu naweza kuwafanya watu waamini! Basi kama hili halijafanikiwa, basi ninamwamini Bwana. . .Nina manyoya ya kondoo mbele Zake, nitarudi, moja kwa moja tu pamoja na ono, moja tu ama mbili ama tatu, ama chochote ninachoweza kupata kwa usiku mmoja.

225 Mmekuwa kwenye mikutano yangu, kila mmoja wenu, hamjawahi kuona moja ya nyakati hizo ila iliyokuwa kamilifu. Itakuambia mahali dhambi yako ilipo. Hilo ndilo jambo pekee linaloweza kufanya. Uponyaji tayari ni wako. Kitu pekee ni, basi, ni dhambi; labda kitu unachofanya maishani, ambacho si sahihi, ama au pe—pepo fulani amekushikilia, ambaye hatakuruhusu kuamini. Sasa, unajua, kama sivyo, Yesu alisema uwongo. "Yote yanawezekana kwake aaminiye." Je, hiyo ni kweli? Basi inakaa ndani yako; si katika Mungu.

226 Kama ningesema hapa, kama ningesema, "Hapa kuna, ikiwa unataka, unahitaji noti ya dola." Nadhani ninayo moja. Vema. Ikiwa kuna noti ya dola, hiyo tayari imetolewa kwa ajili ya mtu mhitaji. Ikiwa ndivyo, ni yako ikiwa utakuja uichukue. Hainibidi kufanya zaidi juu yake, niliiweka pale. Je, hiyo ni kweli?

227 Vema, Yesu, alipokufa, alikuponya. "Alijeruhiwa kwa makosa yako, kwa kupigwa kwake uliponywa," wakati uliopita. Ni juu yako sasa. Njoo uichukue, ni yako. Naamini. "Kwa Jina Langu watatoa pepo." Naamini hilo. Ameniruhusu kufanya jambo hilo hapo awali, na ninaamini ataniruhusu nifanye asubuhi ya leo. Je, unaamini hivyo?

228 Vema, acha tu mwisho hapa urudi moja kwa moja upande *huu*, ninyi nyote hapo chini, ili niweze kuomba; na ninapoomba na kumtoa pepo mchafu, ili watu wapate kurudi kwenye viti vyao kuuzunguka ukuta huo. Tafadhali, ndugu, songeni moja kwa moja *hivi*.

229 Sasa angalia hapa. Kuna manufaa gani ya kucheza huku na huku, na kuamini chochote nusu?

230 Yuko wapi yule mama aliyekuwa kwenye hicho kiti cha magurudumu? Wewe, mama. Nini, kuna faida gani kukaa hapo? Yesu Kristo amekuponya. Hakika, Yeye amekuponya.

231 Nilimwona akiongoza mwa—mwanamke fulani kitambo. Ninaamini ni mwanamume anayesimama hapa akiongoza, labda mke wake pale, yeye ni mlemavu ama chochote kile. Mama, hakuna haja ya wewe kuwa katika hali hiyo.

232 Mama mmoja alisema alikuwa na msichana mdogo hapa, mtoto mdogo, alikuwa na shida fulani, na kila aina ya magonjwa na kadhalika, kiziwi, bubu, na kipofu, chochote kile. Hakuna haja ya kufanya hivyo.

Hebu tuinamishe vichwa vyetu. Nataka uamini.

233 Ee Mungu, Baba yetu wa Mbinguni, ninakuja Kwako asubuhi ya leo kama mtumishi Wako. Bwana, nimelihubiri Neno. Ni Neno Lako, si langu. Nami ninajua ya kwamba Wewe uko hapa kuwaponya watu na kuwapa afya. Ninaamini ya kwamba utafanya jambo hilo, Mungu Mpendwa. Nami nakuomba unirehemu. Bwana, tukitambua ya kwamba maono haya, kitu pekee yawezacho kufanya ni kufichua dhambi za

watu. Lakini, Bwana Mungu, naomba Roho Mtakatifu afanye hivyo sasa hivi. Na afunue, katika kila moyo, kizuizi. Kama kuna dhambi yoyote maishani mwao, basi na isamehewe sasa hivi, Bwana, ninaomba kupitia Jina la Yesu Kristo. Basi jalia hawa, kundi hili hapa leo, wawe kama wale majuzi usiku, jalia kuwe na ukombozi mkamilifu kwa kila mmoja wao. Jalia waponywe asubuhi ya leo, warudi Jumatano usiku, wakiwa na furaha, wakipaza sauti na kushangilia. Tujalie, Baba.

234 Sasa kwa mamlaka ya Neno Lako, ninasonga mbele kuwatoa pepo, kutimiza Neno Lako, katika Jina la Yesu Kristo.

235 Sasa, Shetani, najua unawashikilia watu hawa, kitu cheusi, chenye huzuni, cha kutisha kinachowashikilia, wakisema, "Vema, nitajaribu." Lakini nataka kuzungumza nawe! Ninasimama mahali pao, kati yao na Mungu, asubuhi ya leo. Ninasimama kama mtumishi wa—wa Mwenyezi Mungu. Dhambi zangu zimetoweka, kupitia Damu ya Yesu Kristo, kwa imani ya Kiungu niliyo nayo Kwake kama Mwana wa Mungu. Nami ninadai, na Biblia inadai kwanza, na ninazungumza kama Biblia, kwamba aliharibu kila nguvu ulizopata kuwa nazo, pale Kalvari. Na Biblia inadai kwamba wanafunzi Wake wanapaswa kuendeleza agizo hili alilokuwa nalo hapa duniani, hadi mwisho wa wakati. Nami ni mwanafunzi Wake, kwa hiyo asubuhi ya leo ninakuja kama mwakilishi, mwakilishi wa Yesu Kristo, katika matendo Yake. Nimetumwa mahali Pake. Na wakati wowote ninapomwita mtu huyo, nguvu zako zitavunjika, na mtu huyo atakuwa huru na kutoka hapa na kupata afya. Ninakupa changamoto katika Jina, Jina la Yesu Kristo, kupitia Damu Yake, ninasimama. Na unamwacha kila mtu ninayemwekea mikono yangu. Si katika utakatifu wangu, si kwa jina langu, kwa maana jina langu si kitu kwako; utakatifu wangu si kitu, sina wowote. Lakini hutatambua jina langu, lakini utalitambua "Yesu," nawe utatoka. Nami nazungumza na wewe. Sasa ninaenda kwenye changamoto. Na kama ukijaribu kushikilia yeyote wa watu hawa, laana ya Mungu na ije juu yako. Naomba utoke, uondoe mkono wako kutoka kwa Wakristo hawa. Mkono wako mchafu unaoleta maradhi, unaotesa na kulemaza na kuwaletea maradhi watu hawa, na kuwapa magonjwa, ondoa mkono wako, katika Jina la Yesu Kristo.

236 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]. . .Jina la Yesu Kristo Mwana wa Mungu, nakuomba uinuke katika. . .Jina Lake, ukienda nyumbani mzima kabisa, kumtukuza Mungu. Inuka. Na watu wanaweza kuinua vichwa vyao. [Sehemu tupu kwenye kanda.]

237 Mungu Mwenyezi, Mwanzilishi wa Uzima wa Milele, Mpaji wa kila karama njema, tuma baraka Zako juu ya mtu huyu aliyesimama hapa, huku akijua kuwa hii ndiyo nafasi pekee ya maisha yake kuwa mtu wa kawaida tena. Nyonga zake na viungo vyote vikiwa katika hali hii, juu ya magongo haya ametembea.

Anataka kurudi nyumbani kwake, kushuhudia utukufu wa Mungu; aliendesha gari maili nyingi kufika hapa. Na, Baba, naomba ya kwamba hii itakuwa ndiyo saa atakayosema moyoni mwake, "Ikiwa wengine wanaweza, naweza pia. Nawe ulikufa kwa ajili yangu, kunikomboa, kama vile ulivyowafanyia wengine." Tujalie, Baba.

238 Kwa hiyo, wewe pepo uliyeufanya mwili wake kuwa kilema, ninakuja katika changamoto ya imani dhidi yako, ili kukusahi katika pambano hili. Ninakuapisha kwa Yesu, Mwana wa Mungu, toka ndani ya mtu huyu.

239 Iweni na kicho, kila mahali. Inamshikilia huyo ndugu. Sasa hebu kidogo tu, si ninii yake...Msiwe na wasiwasi tu, marafiki. Uwepo wa Bwana u karibu. Iweni tu na kicho mwezavyo, ndani na nje. Maskini mtu huyo amekuja hapa, hatatembea tena bila magongo ikiwa Mungu hatamsaidia sasa. Hii itakuwa...Akija hapa, atakuwa mbaya kuliko alivyowahi kuwa kama hataponywa. Labda itabidi wambebe ikiwa hajapona. Maana, Shetani, kama anaweza kupata nguvu za kutosha kumwangusha, atamvunja moja kwa moja akiweza. Kwa hiyo sasa ama atamvunja, ama Mungu atamkomboa na kumfanya mzima kabisa. Sasa, kila mtu, ni wangapi hapa ndani wanaoamini ya kwamba Mungu alinituma nimkomboe mtu huyu usiku wa leo kupitia kwa Mwanawe, Kristo Yesu? Vema. Sasa iweni na kicho kabisa, endeleeni kuinamisha vichwa vyenu.

240 Wewe amini kwa moyo wako wote, bwana. Unaamini utachukua magongo haya ya zamani na kuyatupa kwenye gari na kwenda nyumbani, na uyabebe mabegani mwako kesho na utembee huku na huku kwenye barabara za jiji lako, ukimshuhudia Mungu. Hujaninii...Maisha yale uliyobaki nayo, ndugu, yatoe kwa ajili ya utukufu wa Mungu. Je, utamtumikia? Je, utamtumikia? Umekuwa ukifikiria jambo hilo hivi majuzi, hata hivyo, (sivyo?) umekuwa ukifikiria kuhusu kutembea kwa karibu zaidi. Hivi majuzi, ulisema, "Ikiwa mimi...Mungu angeniponya tu, ningetembea karibu Naye zaidi." Hiyo ni kweli. Ulisema hivyo.

241 Halafu, jambo lingine, ulipokuwa...Naona ulikuwa kwenye gari hivi majuzi, nawe ulikuwa unazungumza na mtu fulani kuhusu mambo hayo. Kulikuwa na mtu aliyekuwa ameketi kwenye kiti cha mbele, ambapo ulikuwa umekaa nyuma. Je, hiyo ni kweli? Mlikuwa mnashuka kwenye barabara, mkipita kwenye kifundo kidogo, mkigeukia kulia, mlipokuwa mnazungumza juu yake. Je, hiyo ni kweli? Sisomi mawazo yako, bwana. Huyo ni Mungu sasa. Na sasa unaanza kuhisi kile ninachozungumzia. Sasa ndiyo wakati wa ukombozi wako.

242 Mungu Mwenyezi, sasa wakati nguvu za Uwepo Wako zikiwa hapa, zimesimama hapa kumkomboa mtu huyu, Ee Mungu wa

Milele, Mwanzilishi wa Uzima, tuma baraka Zako juu yake, ninapombariki katika Jina la Mwanao. Tujalie, Bwana, kupitia Yesu Kristo.

243 Ewe pepo uliyemlemaza mtu huyu, ndugu yangu, amefanya maungamo yake. Siri zake zimetajwa. Yuko hapa sasa kutembea. Huwezi kumshikilia tena. Anataka kumtukuza Mungu. Ninakuja katika changamoto dhidi yako. Katika Jina la Yesu Kristo, kwa karama ya uponyaji niliyohudumiwa na Malaika, ninakuapisha kwa Yesu Mwana wa Mungu, toka ndani yake.

Huko, anaondoka. Endeleeni kuinamisha vichwa vyenu, kila mahali.

52-0224 Kumwamini Mungu
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2022 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org